# *MSIOGOPE*

Bwana awabariki. Ni vizuri sana kurudi katika nyumba ya Bwana usiku wa leo, sikuzote nina furaha kuja katika nyumba ya Bwana. Mimi. . . Yapata wakati tunapofahamiana, ndipo wakati wa kuondoka tena umekaribia. Huu mkutano unamalizika kesho usiku, naamini hiyo ni kweli. Lakini ninaamini tunaweza kukaa mpaka Jumapili alasiri. Hiyo ni. . . Ninyi ambao itawabidi kuondoka, ambao ndio kwanza mfanye matayarisho kwa ajili ya kukaa wakati wa mkutano, bila shaka mtafanya mipango ya kuondoka.

2 Nami nilikuwa nikijaribu tu kuzungumza katika mkutano, na kisha kuziweka siku zingine mbili usiku, kuziingiza tu ndani, mikutano mingine miwili, watu wote wapate kuombewa, lakini nasikia ya kwamba baadhi yao hawana budi kuondoka, kwa hiyo tutawaombea wagonjwa usiku wa leo.

3 Na sasa, kama yeyote wenu atakayebaki, tungefurahi sana kuwa pamoja nanyi kwa ajili ya ibada ya Jumamosi usiku, basi tutakuwa na Jumapili alasiri, kwa hiyo hatutaingilia ibada ya mhudumu mwingine yeyote. Nanyi wageni hapa ambao mtasalia huku, sasa jitafutieni baadhi ya hayo makanisa mazuri karibu na hapa, ndugu hawa wanaoshirikiana katika kongamano na mkutano huu, na mjitafutie mahali kwa ajili ya shule ya Jumapili, na muwachukue watoto wenu na kwenda kwenye shule ya Jumapili. Nami nina hakika mtakuwa na makaribisho mazuri, kwa yeyote wa ndugu hawa; kanisa tu utakalochagua.

4 Na kwa hiyo basi, ndipo tutafunga Jumapili alasiri, kuonyesha heshima kwa ndugu zetu ambao wana mikutano yao ya kawaida. Hatuko hapa kwa ajili ya pesa, kwa ajili ya kitu kingine chochote, bali kujaribu kuwasaidia ndugu zetu kuendelea kuusukuma mzigo, kila kitu tu tuwezacho. Halafu pia tunataka kumsaidia kuwaombea wagonjwa, tufanye yote tuwezayo kuwasaidia. Tumekuja hapa kwa kusudi hilo.

5 Na sasa, imekuwa baridi kidogo, na baadhi yao wanalalamika. Yuko wapi mzee rafiki yangu, Ndugu Kidd, usiku wa leo? Mimi. . . [Ndugu fulani anasema, "Nilimwalika hapa juu, Ndugu Branham, bali alitaka kungojea, ama kitu fulani."—Mh.] Vema. Nawaambia! Je, unaweza kunisikia ewe kijana? Vema, hilo ni zuri.

6 Loo, Bwana alimbariki na kumponya, wakati yeye. . . madaktari walidhani atakufa, angali anakaa pamoja nasi. Ninakutaka hapa juu kesho usiku uninukulie wimbo huo uliounukuu nilipokuja kuwatembelea. Unaona? Unajua wimbo huo, niliokwambia nilitaka kuukariri? Kumbuka, nilimwahidi

Bwana huo, kwa hiyo huna budi kuwa hapa kesho usiku, ewe jamaa mdogo. Ninataka uninii . . .

7 Nawaambia, kamwe sitasahau ziara hiyo. Niliondoka nyumbani yapata saa nane usiku, kujaribu kuiharakisha safari yangu sana, maana ilinibidi niondoke, niende mbio kumwona maskini Ndugu Kidd. Nami nikasema, “Je, anaweza kukaa hadi Jumapili?”

Mke wake mpendwa akasema, “Kulingana na madaktari, hatakuwa hapa wakati huo.” Kasema, “A—afadhali uje sasa hivi, Ndugu Branham.”

8 Vema, nikaingia moja kwa moja kwenye gari langu saa nane, nami nilihofu ningeshikwa na usingizi, maana nilikuwa macho hadi karibu usiku wa manane. Nami nikamchukua Billy anisaidie, ndipo tukafika nyumbani. Nami nikaangalia ameketi pale, na maskini jamaa huyu mzee, ni—nilimhurumia sana. Hiyo ni . . . Maskini fimbo ndogo mkononi mwake namna hiyo, ilionekana kwangu kama mzee Yakobo wakati alipokuwa akijiandaa kuondoka, mwajua, na kuwaita watoto waje kando yake.

9 Na mle ndani, kulikuwa na mwanamke, mmoja wa washiriki wa kanisa lake, Ndugu Kidd yuko katika umri wa miaka sabini, nami sijui, huyo mwanamke alikuwa kwenye themanini na kitu, ama labda tisini, mwangavu tu kabisa, umri wa miaka tisini na miwili, tisini na miwili. Ninii tu . . . Mwerevu zaidi kuliko mimi, mwenye akili na mwerevu tu awezavyo kuwa.

10 Miaka tisini na miwili, naye Ndugu Kidd aliyeketi hapa, akamwangalia, akasema, “Nyanya,” naye sabini na kitu, mwajua, “Nyanya, unaonekana kama tone kubwa la theluji asubuhi ya leo.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli, amefanywa safi na mweupe katika Damu ya Mwana-kondoo.”

11 Alionekana ana sabini, na mke wake yapata sabini na kitu, nami nikawazia, “Ninyi wazee mnangojea nini hapa nje asubuhi ya leo, kwa vyovyote vile?” Nikawaza, “Mnangojea tu ule mtumbwi uje, hivyo tu, mvuke mto.” Ni wakati mzuri jinsi gani!

Naye akasema, “Siwezi kukuimbia wimbo, lakini ninataka kukunukulia mmoja.”

Nikasema, “Ndugu Kidd, nataka uninukulie huo jukwaani huko Chautauqua.”

Niliwaona wote wakiangalia kote, “Hivi atakuwa Chautauqua?”

12 “Loo, naam, atakuwako.” Huyu hapa, ameketi hapa usiku wa leo, amekuwa mkutanoni kila usiku. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Asante Bwana mwema.

13 Mambo mengi sana yamesemwa na kufanywa mpaka ninii. . .inanichukua saa kadhaa. Nami najua ya kwamba mnakaribia kuganda huko nje. Nitawaambia, hayuko hapa usiku wa leo, mke wangu, alisema, "Bill, unawagandisha watu hao hata kufa." Kasema, "Wamejizungushia mablanketi huko nje, wengine juu ya kichwa chao. Na huko baadhi yao hata hawajavaa sweta, baadhi ya watu waliokuja hawakuitarajia." Kisha kasema, "Wewe unaendelea tu kuhubiri."

Ndipo nikasema, "Nadhani mradi tu wameketi pale, nitazidi kwenda, kwa hiyo. . . "

14 Vema, ninaamini afadhali niwe na baridi kidogo kuliko vile ningetaka kuwa na joto kupita kiasi kidogo. Kwa hiyo, tunashukuru kwa yale Bwana anayotuma, chochote kile.

15 Sasa, kuwaombea wagonjwa, nitajaribu usiku wa leo kurudi na kuwaita wachache wa hawa watu na kuweka huduma ya kale ya upambanuzi Bwana akipenda, sijui ya kwamba atafanya hivyo. Asipofanya hivyo, basi tutaendelea moja kwa moja kupitia mstarini. Ndipo kesho usiku, tutabadilisha jambo hilo, mnaona, nami nitajaribu kuwaombea wagonjwa kwa njia tofauti kesho usiku, Bwana akipenda.

16 Sasa usiku wa leo, hebu na tufungue Biblia zetu sasa, ninyi mnaoandika hili somo. Kwa dakika chache tu, maana tuna mstari wa maombi, nasi tunataka kuninii. . .Mimi. . .Billy aliniambia tulipokuwa njiani tukienda kwamba aligawa kadi mia moja, nafikiri, alasiri ya leo. Tusingeweza kuwapitisha wote kwenye mstari wa upambanuzi, bali tutawachukua wachache wao. Halafu basi kesho usiku, tuanze jambo lingine, ninaamini litakuwa bora zaidi.

17 Mathayo 14, hebu tuanzie kwenye kifungu cha 22:

> *Mara Yesu akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni, na kutangulia kwenda ng'ambo, wakati Yeye alipokuwa akiwaaga makutano.*
>
> *Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba: Na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake.*
>
> *Na kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana na mawimbi, maana upepo ulikuwa wa mbisho.*
>
> *Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaendea, akienda kwa miguu juu ya bahari.*
>
> *Wanafunzi Wake walipomwona akitembea juu ya bahari wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu.*
>
> *Lakini* mara Yesu. . .*Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msiogope.*

18 Hapana shaka ilikuwa karibu machweo, ilikuwa ni siku ya ajabu sana. Mambo makuu yalikuwa yametukia, walikuwa wameona jambo fulani likitukia ambalo halikuwa limetukia hapo kabla katika historia yote ya ulimwengu. Na kwa kawaida Yesu anapokuwa karibu, unaona mambo yakitukia ambayo ni ya ajabu, ya kipekee.

19 Yule mvuvi mkubwa alikuwa akiweka misuli yake mikubwa na migumu kwenye ile meli ndogo alipokuwa akiisukuma kutoka ufukoni. Watu walikuwa wamekusanyika ufukoni, nao walikuwa wakiwaaga kwaheri wakati akisukuma mashua, gubeti mbele, akaigeuza, akawapungia mikono watu wote ufukoni.

20 Nami ninaweza tu kumwona akitembea na kuketi karibu na Andrea, ndugu yake, akichukua kasia, na kuanza taratibu pamoja na hao ndugu wengine, wakiivuta meli hiyo ndogo walipokuwa wakivuka ziwa. Mara kwa mara, wangesimama, wawapungie mikono hao watu walipokuwa wakimsifu Mungu na kuwaaga, kwa kuwa walikuwa wamepokea amri kutoka kwa Yesu kuvuka ziwa, angekuja baadaye. Naye alikuwa amepanda mlimani kuomba peke yake.

21 Basi hapana shaka kulikuwa na kimya kirefu, kila mtu baada ya kwaheri ya mwisho kusemwa, hapana shaka kulikuwa na kimya kwa muda kidogo. Hakuna mtu aliyesema chochote, huku kila mtu akiinamisha mgongo wake kwenye makasia, na kuivuta ile meli ndogo ilipokuwa ikivuka kwenye bahari shwari, wakati tu jua linapotua. Kila kitu kinaonekana kuwa na amani na utulivu, ni siku ambayo imekwisha.

22 Hivi mmewahi kuona wakati upepo unapovuma kwa nguvu sana, kwa kawaida utasimama karibu tu na wakati jua linapotua? Ajabu jinsi mambo kama hayo yanavyotukia. Huko milimani unapowinda, haidhuru upepo unatoka upande gani, utashuka moja kwa moja mlimani wakati wa mapambazuko, ushuke moja kwa moja mlimani; haidhuru kama upepo unapanda moja kwa moja mlimani, utabadilika na kushuka moja kwa moja wakati siku inapoanza kupambazuka.

23 Mnapenda kuangalia mambo katika maumbile? Hivyo ndivyo unavyomwona Mungu, Yeye amekuzunguka tu pande zote, kila mahali. Mwangalie katika maumbile. Bwana akipenda, kabla sijaondoka nataka kuhubiri juu ya Mungu katika maumbile Yake.

24 Ndipo tunaona, baada ya kimya kirefu na maskini ile bahari ikiwa shwari, na maskini hiyo mashua ikisonga mbele mbio ilipokuwa ikivuka ba—bahari, hapana shaka ilikuwa ni yule kijana Yohana, alikuwa ndiye mdogo wa umri kuliko wanafunzi wote, na takriban, nakisia, wa kuongea, hapana shaka aliachilia kasia lake lijiendeshe dakika moja tu, na kusema kitu kama hiki: “Ndugu, nimeshawishika zaidi sasa kuliko hapo awali maishani mwangu, ya kwamba hatufuati namna fulani ya

mlokole. Nimeshawishika zaidi kuliko hapo awali kwamba Yeye ni kile anachosema ndicho alicho, kwa sababu leo hii wakati alipokuwa amesimama, akiumega mkate huo na kuwalisha hao elfu tano, hivi mliona mwonekano usoni Mwake? Jinsi alivyokuwa mkali, jinsi alivyoonekana kama Yehova amesimama pale," Naye alikuwa ni Yehova amesimama pale, "akiumega huo mkate na kuwalisha watu elfu tano.

25 "Basi haya ndiyo yaliyoingia moyoni mwangu, ndugu, ninaweza kukumbuka zile hadithi nilipokuwa mvulana mdogo tu, mama yangu akisoma kutoka kwenye Maandiko, Neno takatifu. Naye alisoma wakati watu wetu wa kale walipoingia katika nchi hii, kwamba Yehova Mungu mkuu, kwa muda wa miaka arobaini, alioka mikate Mbinguni kila usiku na kuinyeshea ardhini kwa ajili ya watu.

26 "Basi nilipokuwa nikimtazama leo, akichukua kipande cha mkate na kukimega, na kutukabidhi, kila nilipounyosha mkono wangu, nilitetemeka, kwa kuwa ninaangalia na punde tu Yeye alipovunja kipande chake, kipande kingine kilikuwa kimekua kama hicho tu. Alikuwa akipata wapi mkate huo uliopikwa? Na wakati Yeye angevunja samaki, ningeona kipande cha samaki, sio samaki mbichi, samaki aliyepikwa na samaki aliyekolezwa, tayari amekua kufikia wakati angeweza kuurudisha mkono Wake na kuchukua kipande kingine cha samaki.

27 "Hapana shaka ana uhusiano fulani mahali fulani na Yehova, hapana shaka Yeye yuko mahali fulani karibu Naye au ndani Yake. Kwa kuwa hakuna mtu angeweza kufanya hivyo, isipokuwa Mungu alikuwa pamoja Naye. Naye Mtu huyu ambaye watu wanafikiri ni mlokole, nimeshawishika zaidi kuliko hapo awali kwamba Yeye ni Mwana wa Yehova, la sivyo asingeweza kufanya mambo hayo, kwa sababu Yeye anafanya mambo yale yale ambayo Yehova alifanya. Nanyi hivi mnaweza kumkumbuka akisema, pia, ya kwamba 'Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi'?"

28 Hivyo ndivyo mtu anavyothibitishwa. Hivyo ndivyo Mkristo anavyojulikana, ni kwa maisha unayoishi, na kazi unazofanya.

29 Mtu fulani aliniambia, ninaamini ilikuwa jana jioni, kasema, "Ndugu Branham, hizi zinatoka wapi? Unawezaje kwenda kwenye mkutano baada ya mkutano, ukikaa chini ya huo upako, huku hata ishara moja ilimfanya Yesu dhaifu wakati yule mwanamke alipogusa vazi Lake?" Kasema, "Nakuona umesimama kwa saa moja chini ya huo."

30 Nikasema, "Ningetaka kukwambia, hapa ndipo zilipo, hataki niseme jambo hili, lakini ndugu yangu aliyeketi hapa, Gene Goad, mvulana huyo hagusi mkate wala maji kwa siku kadhaa, akifunga na kuomba, huyu hapa Pat Tyler ameketi, ndugu huyu mwingine aliyeketi hapa karibu naye, hao watu wanalala kifudifudi bila chakula wala maji ninapokuwa

mkutanoni, wakiniombea, huko ndiko zinakotoka. Kama hakukuwa na kitu kama hicho, ningedhoofika."

31 Hao ndio wale watu walio nyuma ya pazia, watu wanaoombea nguvu kwa ajili ya ujumbe, hata wanaweka chini kila kitu. Labda hawana karama za kufanya mambo hayo, lakini wanaweka kila jitihada wawezayo kuiunga mkono, na njia pekee wanayoweza kufanya hivyo waijuayo, ni maombi mbele za Mungu na kufunga. Hapo ndipo nguvu zinapokaa, kumwacha mtu fulani akuombee.

32 Ninaweza kumsikia Yohana akisema, "Nilipoutazama uso Wake, ulionekana kuwa ni ile su—sura hasa ya Yehova. Nami nina hakika ya kwamba Yeye ana uhusiano na Mungu, ama, kwa sababu Yeye hufanya kazi za namna ile ile. Niambie wakati wowote mkate ulipoumbwa nje ya mkono wa Mungu, kwa hiyo lazima iwe ni Yehova."

33 Basi hapana shaka ilikuwa ni yule mvuvi mkubwa, Petro, aliyependa kuzungumza, kwa vyovyote vile, huenda alitikisa kichwa chake, na kusema, "Mnajua, wakati Andrea hapa, ndugu yangu mpendwa, ambaye amekuwa mshirika na mvuvi pamoja nami humu baharini kwa miaka mingi, wakati alipohudhuria mkutano wa yule mtu mwitu, wanavyomwita, Yohana, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, naye angekuja kuniambia ya kwamba nabii huyu alinena juu ya Masihi ajaye ambaye alikuwa amekaribia. Siku moja akaingia ndani mbio kiwazimu, na kusema, 'Simoni, leo ilitendeka!'

"'Ati nini ilitendeka?' Nikamwambia.

"'Amekuja, Yesu wa Nazareti, Masihi-Mungu!'

"'Loo, sasa ngoja kidogo, Andrea. Je, huyu mhubiri amewafadhaisha hivi kwa nini?'

34 "'Nilikuwa nimesimama mtoni, nilipomwona kijana Mwanamume akishuka kwenda ufukoni, katika umri wa miaka Yake ya thelathini, kisha akaingia mtoni, na kubatizwa na Yohana. Ndipo alipopanda kutoka majini, niliona Nuru kama nyota ikishuka kutoka Mbinguni. Ilionekana kwangu kama Nguzo ile ile ya Moto ambayo watu wetu waliifuata kupitia nyikani hadi kwenye nchi hii. Ndipo ilipomkaribia, ilipata kitu kama mbawa kama hua, Nayo ikatulia juu Yake, ndipo Sauti ikatoka katika ile Nguzo ya Moto ikisema, 'Huyu ni Mwanangu, mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani Yake.'

35 "Loo, kamwe sitasahau jambo hilo, Andrea." Naye akamkumbatia kwa mkono, akamvuta karibu naye.

36 "Ndipo nikaambatana naye, nami nikawazia, 'Nitamwona Mtu huyu asiye wa kawaida kuliko wote. Yeye ni, hapana shaka ana Tabia isiyo ya kawaida kabisa, kwa sababu ninajua ya kwamba ndugu yangu hapa si mlokole hata kidogo. Aliona

kitu fulani ndani ya Mtu huyo kilichokuwa tofauti, la sivyo asingesisimkwa namna hiyo.'

37 "Kwa hiyo ninakumbuka, kwenye zile siku ziwani hapa pamoja na maskini baba yangu Mfarisayo kabla hajafa."

38 Na hapana shaka ndugu wote walivuta makasia yao kusikiliza yale aliyokuwa akisema.

39 "Nakumbuka baba yangu mzee Mfarisayo aliniambia tulipokuwa tukivua samaki pamoja, akasema, 'Mwanangu, Simoni, sidhani nitamwona Masihi ajaye, ninazeeka, na siku zangu ni chache. Lakini nimewalea mpate kumtafuta Yeye. Sasa, hebu nikufundishe, mwanangu, ili upate kuwa na hakika utajua Masihi huyu ni Nani, kwa sababu kutakuwako na wengi wa uongo watakaoinuka, kutakuwa na mambo mengi makuu yatakayotukia kabla tu ya kuja kwa Masihi huyu halisi, lakini atakuwa na ishara halisi ya Masihi pamoja Naye.

40 "Na hii hapa ishara ambayo utamjua Kwake, kama ni wa kweli ama si wa kweli: Yeye atakuwa ni Nabii, Mungu-Nabii; Yeye atakuwa ni zaidi ya nabii, Yeye atakuwa ni Mungu. Lakini Yeye atakuwa ni Nabii, pia, kwa maana Maandiko yanasema, yale tunayofuata, Simoni, ya kwamba Musa alisema ya kwamba Bwana Mungu wetu atatuondokeshea Nabii kutoka miongoni mwetu aliye kama yeye. Naye atakuwa ndiye kukusanyika kwa watu sasa. Basi unapomwona Masihi akija, ishara ya kwamba Yeye ni Masihi, Yeye atakuwa ni Nabii.

41 "Nanyi mnamtazamia, kwa miaka mia nne sasa hatujawa na manabii, tangu Malaki. Ninaamini ya kwamba ishara inayofuata ya nabii inayoonekana itakuwa ni Masihi. Nawe iangalie, Mwanangu!'

42 "Na mnajua, nilipoambatana na Andrea, hilo liliendelea kujirudia moyoni mwangu, 'Mtazame Masihi huyu, uone kama Huyo Ndiye ambaye Musa alinena habari zake. Atakuwa Mungu-Nabii, nami nitamjua kwa hilo.'"

43 Naye akasema, "Ndugu zangu, nilipoingia Uweponi mwa Yesu wa Nazareti, aliniangalia usoni kwa mara ya kwanza maishani Mwake, na kusema, 'Jina lako ni Simoni.' Nikajua huyo alikuwa ni Masihi. Isitoshe, bali Yeye alimjua maskini baba yangu mtauwa, Yeye alisema, 'Wewe ni mwana wa Yona.'

44 "Hilo lilitosha kwangu, Yohana. Kabla hajaumega mkate ama chochote kile, hilo lilitosha kwangu. Nilijua Yeye alikuwa ni Masihi, kwa sababu Yeye alitoa ishara ya Masihi."

45 Na hapana shaka ilikuwa yapata wakati huo ambapo, labda, Filipo, wakati aliposema, "Nilimfuata Yeye siku moja, nami nikaenda nyumbani Kwake, nikamsikia akinena, nikasikia yale aliyomwambia Simoni, ndipo ni—nikaondoka. Laiti mngaliuona uso wa rafiki yangu niliyeenda kumleta, Nathanaeli.

46 “Sasa, ninajua Nathanaeli alikuwa ni mtu mzuri, alikuwa ni mtu wa kidini, si mwenye shaka, bali alitaka kuwa na hakika. Ndipo nikamwambia, ‘Njoo umwone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu, yule Masihi tunayemtazamia!’

“Naye Ndugu Nathanaeli akaniambia, ‘Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?’”

Akasema, “‘Njoo uone. Njoo uone, njoo ulichunguze mwenyewe.’

47 “Halafu njiani nikamwambia Ndugu Nathanaeli. . .” Na huenda aliacha kupiga makasia, na kusema, “Nathanaeli, unakumbuka hilo?”

“Vizuri sana, Ndugu Filipo, ninakumbuka jambo hilo.”

48 “Nami nikamwambia ya kwamba Masihi huyu alikuwa ametoa ishara ya Masihi, kwamba alikuwa amemwambia Simoni kwamba alikuwa ni nani, na jina lake lilikuwa nani, na jina la baba yake lilikuwa nani. Nami nikamwambia Nathanaeli isingenishangaza kama Yeye angemwambia yeye alikuwa ni nani.

“Akasema, ‘Nitangojea na kutoa uamuzi wangu mwenyewe.’

49 “Basi wakati alipokuja Mbele ya Bwana Yesu, Yesu alimtazama usoni, na kusema, ‘Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!’

50 “Ndugu, laiti mngaliona mwonekano usoni mwake. Mashaka yote yalikuwa yametawanyika, naye akanena upesi na kusema, ‘Rabi, ulipata kunijua lini Wewe? Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana.’

“Akasema, ‘Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.’”

51 Nathanaeli akasimama, na kusema, “Hilo lilitosha kwangu, nikaita na kusema, ‘Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.’ Kwa kuwa nilijua ya kwamba hilo. . . nilijifunza hilo katika Maandiko. Nilijua ya kwamba Masihi huyo angekuwa ni Mungu-Nabii, nami nikaona ya kwamba Huyo alikuwa ndiye huyo Mtu, nilikuwa nimeshawishika kabisa.”

52 Yapata wakati huo, Andrea, hapana shaka ndiye aliyesema, “Ndugu, na sisi sote je? Siku ile tulipokuwa tukipanda kutoka safarini na kukaribia Samaria, nasi tulikuwa nje ya njia yetu ya kawaida ya mahali tulipokuwa tukienda, lakini Yeye alisema alikuwa na haja kupitia Samaria.

53 “Basi ajabu ilikuwa, mbona Yeye akiwa Myahudi atake kupitia kwa jamii ya machotara, Msamaria, ambao wanachukiwa na watu wetu, wanadharauliwa, hatukuwa na ushirika nao hata kidogo? Lakini hata hivyo, Yeye alitaka kupitia Samaria. Naye alikuwa ametwambia hapo awali ya kwamba hakutenda neno asipoonyeshwa na Baba kwanza.

54 "Ndipo basi tulipofika kule, hivi mnakumbuka, ndugu zangu," kasema Andrea, "matendo Yake ya kipekee wakati huo? Hata asingeingia mjini pamoja nasi, aliketi karibu na kisima cha umma nje ya lango, na kusema, 'Ninyi ingieni mkanunue chakula.'

55 "Basi tulipoingia na kununua chakula, basi tulipokuwa njiani tukirudi, mnakumbuka, Yeye alikuwa akizungumza na mwa—mwanamke ambaye tulijua kwamba katika mji huo alikuwa na jina baya.

"Naye alikuwa amemwambia, 'Nipe maji ninywe.'

56 "Naye akasema, 'Si kawaida kwenu Wayahudi kuwaomba Wasamaria fadhili yoyote. Hatuna uhusiano wowote sisi kwa sisi, kwa kuwa kuna ubaguzi.'

"Naye akasema, 'Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye. . .'

57 "Mnakumbuka, ndugu, sote tulikumbatiana kichakani pale kuona ni kitu gani kingetukia, kusikia kile Yeye angemwambia huyu kahaba aliyetengwa na jamii, mwanamke mwenye sifa mbaya. Huyu tunayeamini kuwa ni Mwana wa Mungu angemwambia nini mwanamke kama huyo? Naye alikuwa amesema alitumwa kwa kondoo waliopotea wa Israeli. Yeye atamfanyiaje jambo fulani? Basi kwa nini kijana Mwanamume katika umri Wake, akizungumza na kahaba huko nje peke yao? Kwa hiyo tukajificha tu vichakani, mnakumbuka, kusikia yale yangesemwa."

58 Kisha kasema, "Yeye alisema, 'Kama ungalijua ni Nani unayesema Naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Nami ningekuletea maji, ama, kukupa maji usije hapa kuchota.'

59 "Nayo mazungumzo yakaendelea, na baada ya kitambo kidogo akamwambia, 'Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.'

60 "Vema, tulipoangaliana . . . Yeye . . . Mwanamke mwenye sifa mbaya asingekuwa na mume.

"Naye akasema, 'Sina mume.'

"Akasema, 'Hiyo ni kweli, umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.'

61 "Basi mliuona mwonekano usoni mwake? Alipogeuka upesi, macho yake makubwa meusi yaliangaza aliposema, 'Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua ajapo Masihi, aitwaye Kristo, Yeye atatwambia mambo haya. Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii, atakuwa Ndiye atakayejua siri za mioyo yetu. Lakini u Nani Wewe?'

"Yesu akasema, 'Mimi ninayesema nawe Ndiye.'

62 "Mnakumbuka tusingeweza kumfanya ale? Akaacha mtungi wake wa maji akakimbilia mjini. Wala tusingeweza kumfanya ale. Naye akasema, 'Ninacho chakula msichokijua ninyi.'"

Chakula Chake kilikuwa ni kufanya mapenzi ya Baba Yake aliyemtuma.

63 "Nasi tukashuka kwenda mjini pamoja Naye. Nanyi mnakumbuka? Watu wote wa mji huo, wote waliokuwa katika Samaria, katika mji huo, Sikari, walimwamini Yeye, kwa sababu Yeye alimwambia mwanamke huyo shida yake ilikuwa ni nini."

64 Watasimama katika Siku ya Hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki hapa na kukihukumu, kwa sababu Yesu hajafa, Yeye yu hai milele, yeye yule jana, leo, na hata milele. Alisema ya kwamba malkia wa Kusini angesimama katika siku za mwisho kwenye ile Hukumu na kukihukumu kizazi hicho, kwa sababu alikuja kutoka pande za mwisho za ulimwengu apate kusikia upambanuzi wa Sulemani, ndipo akasema, "Amin, nawaambia, kwamba Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa."

65 Na usiku wa leo, katikati yetu yupo Aliye mkuu kuliko Sulemani, kwa kuwa ni Roho Mtakatifu, Roho Mwenyewe wa Yesu Kristo akijaribu kufanya njia Yake kuingia mioyoni mwa watu na katika maisha fulani. Watu wa huo mji, ndivyo Maandiko yasemavyo, kwamba walimwamini Yeye kwa sababu ya neno la huyo mwanamke.

66 Basi tunapovuka taifa, wakati huduma hii ambayo Yeye amenipa, sasa imeingia katika iliyo kuu zaidi, lakini huduma aliyonipa imethibitishwa tena, na tena, na tena, na tena, nao watu wanabaki wametiwa rangi katika theolojia yao wala hawatasonga hata kidogo. Mwanamke huyo wa Samaria atasimama katika siku za mwisho kwenye Hukumu, na kuihukumu Marekani kwa kutokuamini kwao kwa miaka elfu mbili ya mafundisho ya Biblia.

67 Na bado ni Mungu yeye yule aliyetoa ahadi ile ile, na kusema, "Itakuwa kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu, itakuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma . . . "

68 Siku za Sodoma, kulikuwako na u—uamsho mkuu ulioendelea. Mmoja wa akina Billy Graham wa kisasa alishuka akaenda Sodoma na kuhubiri Injili, wakawa na wakati mzuri sana, na kuwaita waliokuwemo mle ndani. Na hilo lilikuwa kanisa la kawaida na la kimwili, lakini angalieni kilicholipata, liliingia moja kwa moja na kuunda taifa kuu lililoitwa Moabu.

69 Lakini Ibrahimu, yule mteule, kulikuwa na Malaika aliyesimama pamoja naye, pia, na kufanya ishara ile ile ambayo Yesu alifanya, ishara ya Masihi, kamwe hakuwa ameiona hiyo, Ibrahimu. Alikuwa ni mgeni, hao Malaika wawili walikuwa wakienda Sodoma, bali aliketi huku ameelekeza mgongo wake kwenye hema, Naye akasema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" Alijuaje kwamba alikuwa ameoa? Alijuaje alikuwa na mke? Alijuaje jina lake lilikuwa Sara?

Ibrahimu akasema, "Yuko hemani nyuma yako."

70 Akasema, "Ibrahimu, Mimi," *mimi*, kiwakilishi nafsi, "kwa muhula wake nitakuzuru, na mtoto huyu ambaye umeshikilia ahadi Yangu, nitahakikisha ya kwamba amezaliwa."

71 Naye Sara akiwa nyuma Yake, huko nyuma ya upindo wa hema, kwa namna fulani alicheka kichinichini, tungekuita, kafanya, "*Humfu*!" nafsini mwake, akacheka moyoni mwake.

72 Ndipo Malaika huyo akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Haleluya! "Kwa nini Sara akacheka hemani nyuma Yangu?" Hiyo ilikuwa telepathia ya namna gani? Hiyo ilikuwa ni ishara ya namna gani? Ilikuwa ni ishara kwa watu kutoroka upesi, kwa sababu kitu hicho kilikuwa kinaenda kuteketezwa.

73 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu," jambo lile lile. Tunaona moto katika bunduki za Urusi, tunauona kila mahali. Ondokeni Sodoma upesi mwezavyo, mkamkimbilie Bwana Yesu, kwa kuwa saa ya mwisho na iliyojaa rehema Yake imetolewa. Kesho usiku ninataka kuhubiri juu ya jambo fulani kuhusu hilo.

74 Angalieni, Yesu alisema ya kwamba ingekuwa kama hivyo tu katika siku za mwisho. Alipokuwa hapa duniani, Yeye alifanya ishara hiyo mbele ya Wayahudi, mbele ya Wasamaria, bali si Mataifa. Kwa nini? Mataifa hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote. Wayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi, Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi, Naye akawajia, na kuwapa ishara hiyo. Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mataifa wanamtazamia Masihi ajaye, naye Roho Mtakatifu yuko hapa Kanisani sasa akitoa onyo la Masihi ajaye kwa Mataifa.

75 Tuko katika siku za mwisho, mwishoni tu mwa wakati, na hata hivyo, watu hawataki kuliamini. Wengi watasimama moja kwa moja na kuondoka utakaposema lolote kulihusu. Halafu unataka kuniambia ya kwamba Biblia si sahihi kwamba baadhi ya watu wamechaguliwa tangu zamani kwa hukumu? Biblia ilisema walichaguliwa. "Wenye mfano wa utauwa huku wakikana nguvu zake, hao nao mjiepushe nao," Biblia ilisema hivyo. Alisema, "Mpinga Kristo angewapoteza walio Wateule kama yamkini." Tunaishi katika wakati mzuri sana, kabla tu ya Kuja kwa Bwana Yesu.

76 Loo, wakati Simoni na hao wengine walipoendelea, lazima ibilisi aliangalia chini na kusema, "Loo, ninawaona sasa, wameondoka bila yeye. Sasa ni nafasi yangu! Nitasababisha dhoruba iwazamishe chini ya bahari. Sasa ndiyo nafasi yangu ya kuwaondoa wote."

77 Hivyo ndivyo asemavyo hasa sasa; hilo ndilo ninalohofia litakuwa shida ya kanisa letu. Mnaona sana sana ni kama kitu kile kile siku hizi: Tumeenda nje kwa hamaki kwamba ni majengo mangapi mazuri tunayoweza kujenga, ni mangapi

makubwa mno. . . jinsi tunavyoweza kuyapanua vizuri madhehebu yetu, nasi tukaenda kombo bila Yeye.

78 Naye ibilisi anakuja na pepo zake za sumu, kuanzisha uamsho miongoni mwa watu, akisema, "Usiamini hayo ya kimbinguni. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Afadhali uende kwa mtaalamu wa magonjwa ya akili ukachunguzwe akili yako kabla hujawa mmishenari ama mhudumu," upuuzi huo wote wa namna hiyo, uamsho wenye sumu unaojaribu kusema ya kwamba nguvu za Mungu zinazotenda kazi kupitia Kanisa ni lundo la ulokole.

79 Mnajua Biblia ilisema hivi? Yesu alisema, wakati alipokuwa akifanya hizo ishara kule na kuonyesha, akimwambia Nathanaeli mambo yaliyotukia, hao Wayahudi waliosimama pale walisema, "Mtu huyo ni Beelzebuli, yeye ni mpiga ramli. Tunayo namba yake sasa, anasoma mawazo yao, anatumia telepathia ya kiakili."

80 Yesu akawageukia, na kusema, "Nitawasamehe, Mimi, Mwana wa Adamu nitawasamehe hili, lakini atakapokuja Roho Mtakatifu," kwa ajili ya wakati huu, kasema, "neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika Ulimwengu ujao."

81 Wala watu hawalioni. Wana sehemu moja ndogo iliyonyooka ambamo kanisa huchukua namna fulani ya theolojia, nao wanadumu moja kwa moja nayo. Kama nilivyomsikia Ndugu David du Plessis akisema wakati mmoja, yeye huliacha somo lake, akasema, "Sikai kwenye barabara kuu wakati wote, kwa sababu mhubiri wote. . . mahubiri nifanyayo, na watu wote ninaowahubiria hawaishi kwenye barabara kuu, sina budi kushuka kwenye njia kuwachukua."

82 Kwa hiyo labda hivyo ndivyo inavyotubidi kulifanya, kushuka kwenye vichochoro ama njia za kando na kuwashurutisha na kuwalazimisha waingie. Kama kuna jambo lolote linalowezekana, lifanye liwachome sana, hata itawabidi kuliona, ama kuvaa miwani yao nyeusi na kuondoka, kukataa kuliona. Lifanye dhahiri, lithibitishe, Maandiko.

83 Hivyo ndivyo hao ndugu walivyokuwa wakijadili hilo, walijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Yehova, naye Ibrahimu alijua huyo alikuwa ni Yehova.

84 Sasa, unasema, "Yeye alikuwa ni mwanadamu."

85 Ninajua Yeye alikuwa mwanadamu, lakini wakati Ibrahimu, yeye alipaswa kujua, alizungumza Naye, alimwita Bwana Mungu. *Bwana Mungu* ni "Elohimu." Bwana Mungu, Elohimu, Aliye Mkuu Ajitoshelezaye kwa yote, Mwenye Nguvu, Mwenyezi, Yule aishiye peke Yake, huyo Ndiye aliyekuwa amesimama pale akila nyama ya ndama, akinywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, akila siagi na ugali. Mungu Mwenyewe, akithibitisha ya kwamba katika siku za mwisho, kabla ya historia ya ulimwengu kwisha,

kwamba Mungu angejidhihirisha Mwenyewe tena katika mwili wa kibinadamu. Haleluya!

86 Anataka kuja katika mwili wako, anataka kuingia katika mwili wangu na kujidhihirisha Mwenyewe. Alimtuma Mwanawe kufa, Naye akawa kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, na katika hilo angeweza kutusamehe dhambi zetu, apate kuisafisha maskani Yake, na apate kuishi ndani yetu.

87 Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya; hata nyingi kuliko hizi mtazifanya." Yeye alikuwa mmoja tu, sasa Roho Yake imetandazwa kote ulimwenguni. Loo, Mungu anaweza kuwa anaponya hapa, anaweza kuwa anaponya katika Afrika, akiponya katika Asia, akiponya kote ulimwenguni kwa wakati mmoja, kwa sababu Roho Mtakatifu anaifunika dunia nzima. Mungu hufanya hivyo. Loo, Yeye si ni wa ajabu?

88 Ndipo ibilisi akaangalia chini, akasema, "Nina nafasi sasa, wameondoka bila Yeye."

89 Na kama anaweza tu kulifanya kanisa la Kipentekoste lianze kufikiria zaidi juu ya majengo yao na makusanyiko yao yaliyovalia nadhifu, kuliko wanavyofanya kwa mkutano wa maombi wa mtindo wa kale na mkutano wa kukesha, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na maisha ya kitauwa, na wanawake wao kujisafisha, na kuwasafisha wanaume wao, kuwafanya waishi kitakatifu, na ama wafuate nyayo ama watoke, wala si kutegemea pesa sana, na kuombaomba pesa, na kuchanga, muda si muda mwajua, mtajikuta mmeondoka bila Kristo tena.

90 Ndugu, dada, kumbukeni hili: BWANA ASEMA HIVI, unaona, afadhali kanisa lijisafishe! Mnateleza mbali sana. Rudini kwa Bwana, rudini kwenye mikutano halisi ya maombi.

91 Maskini mhubiri rafiki yangu wa Kimethodisti niliyemleta hapa, alilala kwenye chumba hicho hivi majuzi usiku, mpaka saa tisa usiku. Mwanangu akaenda kumwona, alikuwa huko chini mtoni mahali fulani, akiomba, ilimbidi kuingia kazini, mkewe alikuwa tayari amempokea Roho Mtakatifu. Jana usiku alifaulu, nusura apararue mahali hapo, akakimbia na kumchukua ndugu yake na shemeji yake, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Ninawaambia, Wamethodisti wanaenda kutikiswa huko Kentucky katika siku chache. Ni halisi, Roho Mtakatifu wa Mungu, na ni kwa ajili ya Wamethodisti, kwa ajili ya Wabaptisti.

92 Hebu niwaambie ninyi watu wa kimadhehebu hapa, wa Methodisti, Presbiteri, wakati watu hawa hapa wanapojiita Wapentekoste, hilo halimaanishi ni dhehebu, huwezi kuiundia Pentekoste dhehebu. Unaweza kuwa na dhehebu, lakini Pentekoste ni tukio la "yeyote atakaye na aje," kama yeye ni Mbaptisti, Mpresbiteri, Mmethodisti, mweusi, manjano, hudhurungi, ama mweupe.

93 Haileti tofauti yoyote yeye ni wa rangi gani, yeye ni mkubwa jinsi gani, jinsi alivyo mdogo, jinsi alivyo duni, jinsi alivyo mbaya, haileti tofauti hata kidogo, ni kwa yeyote atakaye, ni mchakato wa Mungu wa kulitakasa Kanisa Lake. Haikubidi kuwa mwerevu, si lazima uwe na elimu.

94 Hakuna ila mmoja katika kundi Lake lote aliyepata kuwa na elimu yoyote, huyo alikuwa ni Paulo, naye Paulo alisema ilimbidi kusahau kila kitu alichojua ili kumpata kumpata Kristo. Mungu hajulikani kwa nguvu za kiakili, Mungu anajulikana kwa tukio kupitia kwa Roho Mtakatifu. Petro alikuwa ni mtu asiye na elimu wala maarifa. Lakini ilimbidi kusahau yote aliyowahi kujua, ilimbidi Paulo, kusudi ampate Yesu.

95 Ibilisi aliangalia chini, kasema, "Nimewapata sasa." Ndipo akaanza kupuliza pumzi yake. Basi alipofanya hivyo, bahari ilionekana kana kwamba upande wa chini ungetoka.

96 Ninawazia pepo wake wakisimama kwenye kila wimbi wakasema, "Loo, tumewapata sasa! Tumewapata tu mahali pa kuzamia."

97 Na wakati Wapentekoste walipoanza kutenda, nayo makanisa yao yakaanza kutenda jinsi mnavyofanya, kuingia katika kundi dogo la dhehebu, wakisema, "Tunalipinga kundi *lile*," Church of God dhidi ya Assemblies, Assemblies dhidi ya Church of God, Umoja dhidi ya Uwili, Uwili dhidi ya Utatu, na loo, huo, upuuzi huo wote mbalimbali, mnaona, ibilisi tu, "Nimewatenganisha. Hivyo tu. Nimewaondoa Kwake."

98 "Mmepiga mbio vizuri; ni kitu gani kilichowazuia?" Nini kilitukia? Wanawake wenu wakaanza kukata nywele zao, kutumia rangi ya makucha usoni mwao mwote, na—na kuvaa kila namna. . .Wanaume wenu walifanya nini? Wakaanza kufanya vituko kama kila kitu, wakifanya mizaha, na baadhi yao ni wachafu sana. Mkaanza kuchukua mashemasi waliokuwa na wake wawili au watatu, mambo yote ya namna hii. Ilikuwa ni kitu gani? Mlienda kwa hamaki bila Yeye. Hiyo ni kweli kabisa.

99 Mlipaswa kumweka miongoni mwenu na kuendelea, bali iliwabidi kuwa na kundi kubwa kidogo kuliko lile lingine lililo nalo. Mungu haishi katika makundi makubwa, anaishi katika mioyo minyenyekevu, bila shaka anaishi, ya namna yoyote ya kundi litakalompokea.

100 Una akili bora zaidi. "Loo, hatuna budi. . . " Nimekuwa na wahudumu kuniambia, "Afadhali uende ukamwone, kwa sababu yeye ni mtu mwenye ushawishi katika jiji hili."

101 Sijali kama yeye ni ombaomba mtaani mlevi sana hawezi kusogea, yeye ni sawa tu na meya wa jiji mbele za Mungu, maana ni, "yeyote atakaye, na aje." Lakini tulimtafuta mtu mwingine aliyekuwa bingwa wa sinema, ama aliyekuwa na mvuto mkubwa, ama—ama mcheza dansi la kuchapua miguu, ama yo—yosayosa ya kisasa, ama chochote unachotaka kuliita.

102 Mungu anaenda kwenye mifereji, "Enendeni mitaani na njia kuu, mkawashurutishe kuingia." Basi kumbukeni, huo ulikuwa ndio wito wa mwisho. Kanisa limeondoka bila Yeye, mnaona, mmeingia katika hamaki.

103 Sasa, sipingi dhehebu lolote, Mungu atupe kama elfu moja zaidi, napenda madhehebu. Nina jina la kuwapiga vita, lakini hiyo ni kwa sababu tu watu hawajui Roho wa Mungu. . . Mimi sina chochote dhidi ya madhehebu, mimi si kitu kimoja, niko upande wao, kila moja. Niko pamoja na Assemblies, na pamoja na Church of God, na pamoja na Pentecostal Holiness, pamoja na Umoja, pamoja na United, pamoja na P. A. ya J. C., hao wote, wote ni madhehebu yangu, mimi ni mfuasi wa kila moja la hayo.

104 Lakini, ndugu, mradi tu dhambi iko mle ndani, nitagonga kwa nguvu niwezavyo kwa Injili hii, mpaka nione takataka zimeondolewa, hata ninaweza kuliona Kanisa kuu la Mungu la Mungu wamekumbatiana, wakisahau tofauti zao, wakiziacha dhambi nyuma yao, na kuendelea hata utimilifu, wakiwaondolea mbali akina Tomaso wote, na kadhalika, nami sijali wao ni akina nani. Hiyo ni kweli.

105 Mafuta na maji hayatachanganyikana, kwa hiyo mnapoondoa kutokuamini kwote kutoka kwenu, Mungu ataingia na kuanza kutenda kazi miongoni mwenu. Hiyo ni kweli. Lakini mpaka mtakapofanya hivyo, Yeye hatafanya hivyo, mnateleza na kutoka nje.

106 Sasa, hao wanafunzi katika hali mbaya sana, walikuwa bila Yesu, nao walikuwa huko nje baharini. Lakini walikuwa wakifuata amri, Yesu aliwaambia waondoke, "Enendeni ng'ambo ya bahari, ninaenda kuomba." Nao walikuwa wakifuata kwenye wajibu.

107 Sasa, ndugu zangu, kama mlinichukia dakika chache zilizopita, basi nipungieni mkono sasa. Ungali unaufuata wajibu wako, mradi tu unahubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu na kudumu katika ile Njia, ungali kwenye wajibu.

108 Yesu hakuwa ameenda mbali sana, lakini yale, mnajua yale aliyofanya? Alipanda mlima mrefu kuliko yote iliyokuwamo nchini humo, ili aweze kuona kote kote baharini. Alikuwa amewatuma, alitaka kuona walipoingia katika shida, awe na hakika kama jambo lolote lilitendeka, mbona Yeye angekuwepo kuwasaidia. Angekuwa—angekuwa papo hapo kuwasaidia kama jambo lolote lingetukia.

109 Alipanda juu ya mlima, angeweza kuona kote ng'ambo ya bahari, kote kote ng'ambo ya ile bahari ndogo kule. Ndipo alipoona upepo ulikuwa wa mbisho, Shetani alikuwa akipulizia pumzi yake dhidi yao, halafu basi nini kilitukia? Moja kwa moja katika saa yao ya dhiki kabisa, Yesu akawajia akitembea.

110 Sasa, Mungu ameninii. . . Yesu amefanya jambo lile lile, alipanda juu sana hata angeweza kuona kote ulimwenguni.

Alienda wapi? Alipanda ngome za Kalvari. Alisulubiwa kwa ajili ya dhambi zako, Damu ya mwili Wake ilidondoka ardhini. Lakini Yeye . . . Ndipo walipompeleka kule na kumzika, alifufuka asubuhi ya Pasaka na akaendelea kupanda, kupanda juu, kupita yale maeneo, mwezi, nyota, mpaka akaketi mkono wa kuume wa Ukuu wa Mungu Mbinguni. "Jicho Lake liko juu ya shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia," anakuangalia.

111 Akaenda kote hata Mbinguni, mpaka dunia ingeonekana zaidi kama, labda si kama nukta, ndogo kuliko nyota iliyo ndogo sana, lakini Yeye amesimama pale pale, kama maskini mama tai, na anaangalia kila kitu unachofanya, na kujua kila wazo lililoko moyoni mwako.

112 Jambo ni kwamba, wakati hao wanafunzi katika hiyo saa ya dhiki, ni kitu gani kilichotukia? Walipomwona akija, walimwogopa. Sasa, hilo hasa ndilo tatizo la kanisa usiku wa leo, hujui la kusema juu yake. Sasa, hii imekuwa kama miaka minane ama kumi kote hudumani na kote ulimwenguni. Wanaogopa.

113 Wanasema, "Ingewezekana? Je, inawezekana? Huenda ikawa ni la kigeni kidogo. Ninampenda Ndugu Branham, lakini nitawaambia, sijui, kuna mawazo ya kipekee aliyo nayo."

114 Mradi tu unawazia hilo, afadhali ukae kitini mwako. Hiyo ni kweli, kweli. Kuhusu Ndugu Branham mwenyewe, yeye si kitu. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini ninamwakilisha Roho wa kweli wa Mungu, kwa sababu Yeye huja kwa Neno na hufanya yale Neno linayosema yafanywe. Kama hamwezi kuniamini mimi, basi aminini Injili ninayohubiri, sasa, fanyeni hivyo.

115 Yesu alisema jambo lile lile, "Kama inafanya kazi za Mungu, basi ni ya Mungu," maana hakuna mtu anayeweza kufanya kazi za Mungu, isipokuwa Mungu yu pamoja naye ama ndani yake.

116 Sasa, ninawatakeni mwone jambo fulani, waliogopa, wakasema, "Huo unaonekana kama mzuka." Walisema ilikuwa ni roho, hakika ilikuwa ni roho. Walidhani Yeye alikuwa ni roho.

117 Hivyo ndivyo ilivyo usiku wa leo, wanahofu ni roho mbaya, hawajui ni nini kulihusu. Wasema, "Vema, kama angekuwa ni mfuasi wa dhehebu letu, tungelikubali."

118 Loo, maskini dhehebu lenu dogo! Mnaona? Msipoangalia, litawazuia kuingia Mbinguni moja ya siku hizi. Mnalitegemea hilo kupita kiasi.

119 Sasa, kumbukemi, kaeni ndani yake, bali muwe nuru angavu, inayoangaza mle, muishi maisha yasiyo na lawama. Sijali wewe ni wa dhehebu gani, bali usiliegemee hilo sana, egemea msalabani, egemea juu ya Yesu, ndiko unakotaka kuegemea. Sipendi huku kuegemea msalabani, ninataka kuegemea juu ya Yesu.

120 Ng'ambo, sijui ni watu wangapi mbalimbali walio na mihemuko, mwajua, na mambo wanayotaka kufanya. Ninaamini

huko ng'ambo sasa, wana misumari asili kumi na tisa iliyokuwa msalabani. Kila mtu anataka kupeperusha msumari, "*Huu* ndio, *huu* ndio." Mtu fulani ana kipande cha msalaba. Hapa si muda mrefu uliopita, papa mmoja alisimama na alikuwa na kipande cha mbao karibu *hivyo*, akakipeperusha, kasema, "*Hiki* ndicho, *hiki* ndicho."

121 Nilipokuwa Rumi, nilishuka kwenda kwenye kanisa moja ambako wanawachukua watawa wote wanaokufa, na kuwazika mle mpaka nyama ziwatoke, kisha wachukue mifupa yao, na kutengeneza vidole vinavyoshikilia balbu za taa na—na yote namna hiyo, na mifupa pande zote. Nao watu wanaosafiri kupitia kule wameisugua mifupa hiyo mpaka imekuwa, baadhi ya mafuvu ya kichwa yanateleza. Na kulikuwako na sanamu ya Mtakatifu Petro, wengi sana wamebusu kidole chake cha mguu na kukisugua, mpaka imewabidi kuweka futi mbili ama tatu kwenye hiyo sanamu; daima wanagusa, wanasugua.

122 Loo, jamani, liondokeeni! "Mungu ni Roho, nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na katika Kweli. Neno Lako ni Kweli." Roho huja na kulishuhudia Neno. Ndipo ajapo, mnasema, "Loo, ni mzuka," kisha unasugua fuvu la kichwa cha mtu fulani, kisha useme Huyo anaonekana ni mzuka. Mnaona? Hiyo ni . . . Haya basi. Unaona? Unaenda kwenye madhabahu fulani matakatifu, ama ninii . . .

123 Nilikuwa huko La Salle, Lorraine, ama, samahani, la, ilikuwa Notre Dame huko Paris, kulikuwa na mwanamke, mwanamke fulani aliyekufa pale. Nao walikuwa—walikuwa na ma—mahali pale ambapo walikuwa wakipeleka, wakisugua mikono yao juu chini juu ya kichwa chake pale ambapo, alikuwa ndani ya jeneza, nao, namna fulani ya kutiwa dawa asioze, mama huyo alikuwa ametiwa dawa asioze, nao—nao walikuwa wakisugua-sugua pale, wakasema ilizuia majanga yasiingie mjini. Wakati damu ya mwanamke, mafuta kutoka katika mkono wa mwanamume, ama chochote kile kinapochukua mahali pa Yesu Kristo, Damu ya Yesu Kristo, ni upinga-Kristo. Nanyi kumbukeni tu jambo hilo, ni upinga-Kristo.

124 Yesu Kristo ndiye Mpatanishi pekee kati ya Mungu na wanadamu, Damu Yake ilimwagwa mara moja tu, alichukua Damu Yake Mwenyewe, na kuingia katika madhabahu ya Mungu, na kuketi mkono wa kuume wa Mungu, Yeye ndiye Mpatanishi pekee, Yeye ndiye Mwombezi pekee, Yeye ndiye Damu pekee, Roho wa pekee ni Roho Mtakatifu, nami ninaamini kwa yote yaliyo ndani yangu. Hiyo ni kweli. Kibadala chochote chake, kwangu mimi ni kosa, mhemuko wa namna yoyote si sahihi, haina budi kuwa ni Roho. Naye Roho aliye ndani yako anakufanya uishi yale maisha, na kufanya na kutenda kazi za Mungu. Kama sivyo . . .

125 Kama ukiweka roho ya mche wa boga ndani ya mzabibu,

ungezaa maboga. Kabisa, maana ni tunda la mche, aina ya uhai ulio ndani yake. Ukiweka mpichi—mpichi na kuondoa uhai kutoka kwa mpichi, na kuuweka kwenye mkuyu, ungezaa mapichi. Naam, bwana. Kwa sababu ni uhai wa mpichi ndani yake.

126 Mkirudisha Uhai wa Yesu Kristo kanisani, mtaacha kuzozana, mtakuwa ndugu na dada, ninyi wanawake mtaacha nywele zenu zikue, mtaachana na vipodozi, mtazima vipindi hivi vichafu vya televisheni ambavyo havipaswi kusikilizwa, mtaharakisha kwenda kanisani kila Jumatano usiku, mikutano ya maombi itaendelea tu kote mjini, kila mahali, nalo kanisa litakuwa moja katika Kristo Yesu.

127 "Nao Utukufu wa Bwana utarudi, na utakuja Sayuni ukiimba pamoja na furaha kuu." Na kutakuwako na uamsho utakaoibuka kote nchini ambao ungemwaibisha kila mkosoaji, nguvu za Mungu zitaingia kanisani, naye Yesu atakuja na kujidhihirisha Mwenyewe katika ishara kuu na maajabu na karama. Ni kwenye siku ya mwisho tu, akingojea Kanisa Lake liwe katika hali nzuri. Amina. Msiogope hilo, likubalini.

128 Hiyo ilikuwa ndiyo njia yao pekee ya wokovu, ibilisi angewaua papo hapo, angaliwasonga, kama isingalikuwa ni kwa ajili ya Hilo, lilionekana kama mzuka kwao, kidogo lilionekana la kigeni. Na usiku wa leo, tumaini pekee la kanisa ni kuachana na theolojia zao za kujibunia, na kumrudia Roho Mtakatifu, na kumrudisha Roho kanisani, na kulinyosha kanisa, ndilo tumaini pekee la wokovu, ni kumrudia Roho Mtakatifu tena. Amina.

129 Hiyo inaweza kuwa kali sana. Mama yangu alizoea, nilisema alizoea kuniambia. . . Kama kuna kitu ninachochukia ni mafuta ya mbarika. Hiyo ndiyo sababu mimi huuahirisha sana uchunguzi wa kwenda ng'ambo kadiri niwezavyo, maana inakubidi kufanyiwa. Nayo yananikera hata kufa. Lakini akasema, "Chochote ambacho hakikuchefui, hakikufai chochote." Kwa hiyo nadhani kidogo hii inatusaidia, mwajua. Naam.

130 Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu wa Mungu yuko miongoni mwetu, Yeye anajithibitisha Mwenyewe pamoja nasi. Yeye hajafa, Yeye yu hai.

131 Wakati mmoja, walimjia, na kusema, "Bwana, sisi tunataka kuona ishara."

132 Yeye alisema, "Kizazi dhaifu na cha zinaa chatafuta ishara."

133 Na kama hicho sicho kizazi tunachoishi ndani yake, kamwe sikukijua. Kizazi kiovu na cha zinaa, kile tulicho nacho sasa. Angalieni uzinzi, angalieni talaka. Talaka, visa vya talaka vya Marekani vimeenea ulimwengu mzima. Bila shaka, vimeenea, hakika vimeenea. Ndizo mbaya kuliko zote zilizoko ulimwenguni, ni talaka. Wanawake wetu wameachiliwa huru,

wakikimbia kama kundi la nguruwe mwitu. Sasa, hiyo ni kweli kabisa, wameachiliwa huru.

134 Hakimu anafanya nini? Anakuruhusia talaka yako. Biblia ilisema, "Wote aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe." Siamini katika talaka. La, bwana. Mungu huwaweka wanaume, wanawake pamoja, nao wanapaswa kuishi hivyo maishani mwao mwote.

135 Na watu wetu wa Kipentekoste, wakiwachukua hao wanaume waliotalikiwa, wakiishi na wanawake wawili ama watatu mbalimbali, na kadhalika, na kuwafanya mashemasi kanisani, na kadhalika. Hmm! Ni aibu! Ni fedheha kwa Jina la Yesu.

136 Kama vile, ninaamini ilikuwa huko India hivi majuzi, walisema, "Upelekeni mbali Ukristo wenu, hatuutaki. Tungependa kumjua Yesu, lakini hatuutaki Ukristo wenu, ni mbaya sana." Mbona, huko India ambako kuna aina arobaini ama hamsini mbalimbali za dini, wanaweza kutufanya tujionee aibu.

137 Na Wahotentoti huko Afrika, katika moja ya hayo makabila, sijui kama ni Wazulu, Washangaan, ambao ndio, kuna moja ya hayo makabila ambalo lina mila kali sana, kwamba kabla mwanamke hajaolewa hana budi kuchunguzwa ubikira wake. Kama akipatikana na hatia, hana budi kutaja mwanamume ambaye amefanya hivyo, na wote wawili wanauawa pamoja. Hakuna uzururaji wa usiku katika kabila hilo.

138 Vipi kama tungefanya hivyo Marekani? Mngewazika wapi hao wote? Mnaona? Haya basi. Wanaweza kutuambia maadili, jinsi ya kuyaishi, hata hivyo tunapaswa kuwa watu watakatifu walio na Roho Mtakatifu. Tunaachilia uozo kama huo uingie kanisani mwetu, ni dhambi na aibu. Mungu aturehemu.

139 Ndipo Roho Mtakatifu anakuja, anatenda kazi na kuonyesha ishara Zake, nao wanaondoka tu kana kwamba "Vema, nadhani ilikuwa ni sawa." Loo, kana kwamba umekufa nusu.

140 Mwaminini Mungu. Amkeni! Kufa kotekote, kusudi aweze kufufuka tena. Hivi hamuamini hiyo ni kweli? Saa hii yenye giza, wakati mkuu tunaoishi. Naam, bwana.

141 Sipendi kuwaudhi, Mungu anajua hilo, lakini kile ninachojaribu kusema, kuna wahubiri wanaoketi hapa, mamia yao, labda, katika huu mkutano, kuna washiriki wa kanisa hapa, kile ninachowataka mfanye, ni kurudi kanisani mwenu na kuingia kazini. Hiyo. . .Hatuwezi kufanya hivyo, hatuna budi kukusanyika pamoja, na hatuna budi kuanzisha hili, jambo fulani halina budi kutukia, ndugu zangu. Imefikia mahali, ambapo hicho kitu kinaanguka. Hebu tuanze.

142 Mnajua kinachotendeka? Mungu anainuka kutoka kwa Wamethodisti, Wapresbiteri, Wabaptisti, Walutheri,

wakimpokea Roho Mtakatifu, wakitoka moja kwa moja. Loo, ndugu, angalia, "Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Wanaliona, wanaliangalia, wanalichunguza katika Maandiko, wanasema, "Hayo ni Maandiko, ninayaamini kwa moyo wangu wote," wanatoka moja kwa moja na kumpokea. Mnaona?

143 Kumbukeni, kikosi cha kwanza kilichoanza kuvuka kwenda kwenye nchi ya ahadi kilishindwa, kikafa nyikani, isipokuwa wachache sana kati yao. Kizazi cha pili ndicho kilichoingia kwenye nchi ya ahadi. Mnaona, vitu vyote ni mifano.

144 Sasa, tunakuwa wakaidi sana, "Loo, sisi ni Wapentekoste." "Sisi ni Utakatifu." Loo, hakika. Haya basi, mnaona mahali mnapofikia? Mnaingia mahali fulani, ndipo Mungu anapoanza kutembea na Roho Wake, mnasema, "Ah, ah! Hatujawahi kuona jambo hilo katika siku zetu, kaeni mbali nalo." Mnaona?

145 Angalieni nyuma na kuyachunguza Maandiko, Yesu alisema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini Maneno ambayo Mimi. . .hamwezi kuamini Maneno nisemayo, aminini kazi nizifanyazo, ndipo mtakuwa na Uzima. Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yachunguzeni Maandiko kwa kuwa yanashuhudia, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele." Mnao endapo mtayatii Maandiko. Maandiko yanaposema jambo lolote, basi tiini hilo.

146 Sasa, sana. . .Nilifikiri nitakuwa nimeondoka kufikia wakati huu, bali ninajisikia tu kama kuhubiri sasa, kwa namna fulani nilibadilisha tu nia yangu. Lakini sikilizeni, tuko hapa kwa ajili ya ibada ya maombi kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka.

147 Ndipo wakapiga mayowe, nao waliogopa, ndipo Yesu akanena, na kusema, "Msiogope; Ni Mimi. Msiogope."

148 Sasa, tungejuaje usiku wa leo kama ilikuwa ni Yeye? Kwa sababu Yeye atafanya kazi ile ile aliyofanya. Kama Yeye ni Kuhani Mkuu. . .Waebrania 4:15 ilisema kwamba "Yesu Kristo ndiye Kuhani Mkuu sasa hivi anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Mnaona? Anafanya maombezi. Yesu aliahidi katika siku za mwisho mambo haya yangetukia.

149 Mliamini katika kumpokea Roho Mtakatifu, mkampokea; walimwamini Yesu na kumpokea, walikuwa huko nje baharini tayari kuzama kwa sababu Yeye hakuwako, wakati alipokuja, walimwogopa, kwa sababu alikuja katika umbo tofauti, alitokea kwa njia tofauti, bali ingali ilikuwa ni Yesu. Na ukitaka kujua kama ni Yeye au la, rudi uone kama Neno linasema ni Yeye au la. Lijaribu kwa Neno, Neno humshuhudia Mungu, nalo Neno la Mungu hujishuhudia Lenyewe.

150 Sasa, kumalizia mchezo wetu mdogo wa kuigiza: Hao ndugu walijua, Yohana alijua ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi.

Alijua ingeweza tu kuwa ni Mungu ambaye angeweza kufanya hivyo. Kwa sababu gani? Alikuwa ameona katika Maandiko ya kwamba Mungu Ndiye aliyeioka ile mikate, na kuimega, na—na kuwalisha watu milioni mbili usiku kucha, alijua Huyo alikuwa ni Mungu. Petro alijua ilikuwa ni Mungu, kwa sababu alikuwa amesikia kwamba Masihi atakuwa Mungu-Nabii; Nathanaeli, vivyo hivyo.

151 Yule mwanamke huko Samaria alikuwa amefundishwa, alijua, alisema, "Ninajua ajapo Masihi, sote tunajua jambo hilo hapa Samaria, tunajua Masihi atakapokuja, hayo ndiyo mambo atakayofanya. Lakini u Nani Wewe?"

Yesu akasema, "Mimi Ndiye."

Hakuogopa, alilikumbatia, naye akaenda kufanya jambo fulani kulihusu.

152 Tutamwona akipanda juu ya kusanyiko, akifanya jambo ambalo ni bora sana, akithibitisha kwamba ni Roho yeye yule aliyekuwa juu Yake yuko juu yetu, ndipo tutaondoka, na kusema, "Vema, sijui la kuwazia juu yake." Mnaona? Hiyo ndiyo inayofanya sehemu ngumu. Mungu aturehemu. Jalia isiwe hivyo tangu saa hii na kuendelea, Mungu na awasaidie, Mungu na awabariki.

153 Mungu na anisaidie, nina umri wa miaka hamsini, sina muda mrefu zaidi wa kuwa hapa, kulingana na umri. Kama nikihubiri miaka mingine ishirini, ambapo siamini miaka ishirini itatimia kabla Yesu hajaja. Sasa, sasa hebu, hebu nipate hilo hapa chini vizuri, hebu nilisahihishe hilo: sijui Yeye atakuja lini, lakini inavyoonekana, haiwezi kuenda mbali zaidi, haiwezi kuenda mbali zaidi. Huenda ikawa kabla ya asubuhi, Yeye anaweza kuja kwa ajili yetu papa hapa katika dakika moja ama mbili zifuatazo. Sijui ni lini moyo wangu utakaposimama, au wako utakaposimama, ndipo itubidi kuondoka.

154 Lakini hata hivyo, ninaamini kule Kuja kwa pili kwa Kristo kumekaribia sana, mpaka karne hii ya ishirini haitaisha. Kila kitu kinatendeka. . .Mungu aliujenga ulimwengu katika miaka elfu sita, elfu moja ingekuwa siku moja, kama Maandiko yasemavyo, kila baada ya miaka elfu mbili, jambo fulani limetukia ulimwenguni.

155 Miaka elfu mbili ya kwanza, Nuhu alijenga safina, gharika ikaja; miaka elfu mbili ya pili, Kristo akaja; hii ni elfu moja mia tisa na sitini, na "Nitafupisha kazi kwa ajili ya Wateule, la sivyo hakuna mwenye mwili atakayeokolewa." Haya basi. "Kwa hiyo mtakapoona mambo haya yakianza kutimia, inueni kichwa chenu, kwa kuwa ukombozi wenu unakaribia." Kwamba atakuja lini, sijui. Ila ninajua jambo moja, Yeye yupo hapa usiku wa leo katika umbo la Roho Mtakatifu, Yeye yuko ndani yetu kuamini. Mungu na atusaidie tunapowaombea wagonjwa.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi.

156 Mpendwa Yesu, mimi ni mtumishi wako. Ninataka kuwa mkweli, baada ya kuona ono hilo hivi majuzi asubuhi, ninataka kuwa mkweli zaidi kuliko hapo awali, nikijua jambo hili, ya kwamba sijui ni wakati gani Wewe utaniita, nami itanibidi kukujibu.

157 Sasa, Baba Mungu, kwa karama ya Kiungu ambayo imedhihirishwa kote ulimwenguni, nimefanya vizuri sana nilivyojua, sasa Wewe umeahidi kwamba ingekuwa kubwa zaidi. Nina furaha sana kwamba Wewe unadhihirisha hilo kwetu, kama tutakavyoona mwishoni mwa juma hili.

158 Sasa, Baba, ninaomba, usiku wa leo, ya kwamba utamjalia wokovu kila mwenye dhambi aliye hapa, jalia uponyaji wa Kiungu kwa kila mtu aliye hapa ambaye ni mgonjwa, mpe kila mmoja anayemtafuta Roho Mtakatifu ubatizo usiku wa leo. Mbariki kila mhudumu, kila dhehebu, kila shirika, kila kanisa, kila mmoja anayelitaja Jina Lako. Bwana, jalia wapokee baraka kutoka kwa Mungu.

159 Hata kama kuna wakosoaji fulani hapa, tunawaombea, kwamba wasiwe wakosoaji. Hawamaanishi kuwa hivyo, Baba, wasamehe kwa kuwa wakosoaji, hawakusudii kuwa hivyo. Ninaomba ya kwamba utawajaza sana na Roho Mtakatifu, hata wao, pia, watakuwa washirika pamoja nasi katika huduma ya huku Kuja kwa Bwana Yesu. Tujalie, Baba.

160 Mimi—mimi kwa unyenyekevu, si mbele ya watu, sizungumzi nao, Baba, ingawa mimi. . .wanaisikia sauti yangu, bali ninazungumza na Wewe, kwa uaminifu moyoni mwangu, ninaomba kwa ajili ya kila mtu ambaye angekuwa mkosoaji, kwamba Wewe utawasamehe, na kuwaokoa, Bwana, na kuwapa kazi za Mungu kuifuata huduma yao. Tujalie.

161 Bariki kila dhehebu, jalia kuwe na uamsho utakaotokea miongoni mwa kila mmoja wao, Bwana. Jalia makanisa yao yakue, washiriki wao wakue, nguvu za kiroho zikue. Bwana, tunataka kuona jambo moja: Mungu wetu katika amani. Tusaidie, Baba. Lakini, iwe. . .Tutie mafuta, Bwana, ili tusiwe wazembe, tusiwe wasio na msimamo, tusiwe kundi la mabuu, bali tutakuwa wanadamu, watu waliojazwa na Roho Mtakatifu, kama Petro. Hata hivyo alikuwa asiye na elimu, wala maarifa, ilibidi watambue, yeye alikuwa pamoja na Yesu, kasema, “Tumsikilize nani, nyinyi ama Mungu?”

162 Ee Mungu, utupe watu kama hao leo, watakaolichukua Neno na kulihubiri, na kusema, “Roho Mtakatifu ni wa kweli, na nguvu za Mungu ni za kweli, kule kuja kwa Yesu hivi karibuni ni kweli.” Nao watasimama juu yake kwa ushujaa. . .Tujalie, Bwana. Yasikie maombi yetu.

163 Waponye wagonjwa sasa, na wanaoteseka, na ujipatie Mwenyewe utukufu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Na jalia kila mwenye dhambi aliye hapa, Bwana, ibada

itakapoanza . . . Naomba uje unisaidie, nitakuwa hoi kabisa bila Wewe kunisaidia, ninakutafuta Wewe unisaidie. Tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

164 Nitawaomba ninyi nyote mwendelee tu kuketi, na mtakaposimama, iweni na kicho kabisa. Ningeweza kusimama hapa na kuhubiri mpaka nywele chache nilizo nazo zianguke, ningeweza kusimama hapa mpaka waingie mvi, ama ningezama mimbarani na kufa, ungali ungeweza kusimama hapo, na kusema, "Vema, sijui kuhusu hilo, yeye alilihubiri, bali ningetaka kuliona likitenda kazi."

165 Hiyo ni kweli kabisa. Kama ni ahadi ya Mungu, itafanya kazi. Kama ni . . . Kila ahadi aliyotoa Mungu itatenda kazi kama una imani ya kutosha kuifanya itende kazi.

166 Sasa, sasa, ni—ninawahesabu ninyi nyote kama—kama rafiki zangu, na ndugu zangu na dada zangu ninaotarajia kukaa nao Milele Utukufuni. Na kama hukubaliani nami juu ya mafundisho yangu, hilo ni sawa kabisa, lakini ninaamini kama utaichunguza Biblia yako vizuri kweli, utaona kwamba ni—ni sahihi kabisa. Kwa sababu kwanza, Malaika wa Bwana alinijia na kunifundisha, kisha akanionyesha katika Biblia mahali pa kuyapata. Sina budi kumpata mtu wa kwanza anayeweza kuyakosoa, na hiyo imekuwa kwa miaka mingi. Ni—ni ya kweli, naam, bwana.

167 Baadhi ya wanatheolojia mashuhuri, ambao nimezungumza nao, hatimaye inapofikia kwenye shindano la kuamua, wanasema, "Tunajua ni ya kweli, lakini kanisa letu lingetufukuza kama tungekubali hilo."

168 Vema, kama unawazia zaidi juu ya kanisa kuliko unavyowazia juu ya Kristo, hiyo ni juu yako. Unaona? Lakini kwangu mimi, ninasimama juu ya Neno, katika pengo kati ya madhehebu yote nikisema, "Sisi ni ndugu, sisi ni dada. Hebu tuje tukamtumikie Bwana Yesu." Amina. Hilo ndilo ninii langu—hilo ndilo lengo langu, hiyo ndiyo nia yangu katika kufanya hivyo, ni kuwa safi mbele za Mungu, huo ni moyo wangu wote.

169 Sasa, ninaamini Billy alisema aligawa kadi mia moja moja za maombi. Hiyo ni kweli, Billy? Je, kulikuwa na idadi fulani, ama ninii fulani yoyote . . . ? A. Za A, za A. Kadi za maombi A.

170 Sasa, tutamwombea kila mmoja wenu. Huenda tusiweze kuwapata wote usiku wa leo, tutafanya vizuri tuwezavyo, tushuke mstarini kadiri tuwezavyo. Vema? Itatubidi kuwapanga mstarini sasa, na . . .

171 Vipi kuhusu wewe kushuka hapa chini? Wewe na Gene, ama baadhi yenu, ama mtu fulani unaweza . . . Je, una mtu fulani huko chini angekusaidia? Shuka uende huko chini. Ndugu Sullivan, wachukue kutoka mwisho huo wa mstari, na mtu fulani ashuke pale chini. Ni—nitaangalia ni wangapi wanaoweza kuwapanga mstarini kwanza, na halafu mimi . . .

172 Vema, hebu tuone, hebu na tuchukue namba moja. Waweza kuinua mkono wako uliye na kadi ya maombi namba moja? Namba moja, ninaiona? Ni nini . . .? Una hakika ulikuwa . . .? Ati nini? Ngoja, na—nafikiri amenipa kitu kisicho. Je, wewe . . .? Ulianza . . .? Loo, samahani. Vema.

173 Vema, mama, *hapa*, namba moja. Njoo uwalete kutoka *hapa*. Daima napenda wakitokea upande wa kulia, maana Yeye husimama mkono wangu wa kuume. Mnaona? Vema. Njoo huku upande *huu*. Ninachukia kuwaleta upande huo, lakini si ushirikina. Sasa, kila wakati anapotokea, Yeye yuko upande *huu*, ninawatakeni mkutane Naye kabla hamjakutana nami.

174 Namba moja. Namba mbili, namba mbili. Ni wangapi wanaojua ya kwamba huo si ushirikina? Hilo hata ni la Kimaandiko. Kweli kabisa. Hivi yule Malaika alikuwa amesimama wapi wakati Zakaria aliponena naye, ama, aliponena na Zakaria? Vema.

175 Namba moja, namba mbili. Namba mbili ni nani? Vema. Namba tatu, upesi sasa, namba tatu, inua mkono wako. Namba tatu, namba nne. Kama huwezi kusimama, mwambie bawabu, tutakuja kukuchukua. Namba nne, kadi ya maombi namba nne. Moja, mbili, tatu. Hiyo ni namba nne?

176 Namba tano. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba tano? Njoo upesi. Kadi ya maombi namba tano. Kama mngeinua mikono yenu, ingetusaidia sana. Kadi ya maombi namba tano, ime—imetoka nje? Je, wao . . .? Je, jambo fulani lilitukia? Ameondoka, ama . . .? Loo, samahani, sawa. Nenda moja kwa moja . . . Samahani, bwana.

177 Namba sita, namba saba. Jambo ndilo hilo, hiyo ndiyo njia. Namba nane, namba tisa, namba kumi. Sasa tunakuja. Kumi na moja, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, saba- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

178 . . . Yesu kukuponya? Inua mkono wako. Vema, sasa katika Biblia, haya ndiyo yaliyotukia: Kulikuwa na mama aliyekuja kwenye mstari wa maombi, tutasema hakuwa na kadi, Yesu alikuwa akipita, alikuwa anatokwa na damu, kwa hiyo akagusa upindo wa vazi Lake, na, kwa kuwa alisema moyoni mwake . . . Huenda ilimbidi kutambaa katikati ya miguu yao mpaka akagusa upindo wa vazi.

179 Ndipo akasema basi wakati alipofanya hivyo, alijisikia moyoni mwake ya kwamba imani yake ilikuwa imeridhika, kwamba alikuwa ameponywa, akarudi na kuketi chini na, ama akasimama, ama vyovyote alivyokuwa kwenye kusanyiko.

180 Ndipo Yesu akasimama, na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Ni wangapi wanaokumbuka Maandiko hayo? Hakika. "Ni nani aliyenigusa?" Hakuna mtu aliyesema neno, Naye akaangalia kote. Kwa nini? Nguvu zote za upambanuzi zilikuwa ndani Yake.

181 Sasa, wakati alipougusa ule mwili, sasa, hapa kwa ajili yenu watu, wakati alipougusa mwili Wake, Yeye alikuwa mwanadamu, Yeye—Yeye asingeweza kuuhisi. Alikuwa amevaa vazi, vazi la Kipalestina lina vazi la ndani, linapwaya, joho linapwaya, kwa hiyo, akaugusa upindo wa vazi Lake.

182 Sasa, nisingeweza kutambua hilo kimwili kama ungegusa ncha ya koti langu. Vipi kuhusu lile vazi la Kipalestina lililopwaya sana? Walikuwa na vazi la ndani lililokuwa karibu na miguu yao hapa, kwa sababu wakitembea barabarani waliokota mavumbi, nao wakajaa mavumbi na wachafu sana. Walikuwa na vazi la ndani, kwa hiyo joho hilo. . . Mnaona, Yeye asingeweza kuuhisi kimwili. Lakini hakumgusa Yeye, alimgusa Mungu, wakati alipotamka kwamba aliamini ya kwamba Huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu.

183 Akasema, hapana shaka, "Ninamwamini Mtu huyo, sijali yale kasisi asemayo, ama mtu mwingine yeyote, ninamwamini Mtu huyo. Kama ninaweza kumgusa, nitakuwa mzima." Ni wangapi wanaojua hayo ni Maandiko katika Biblia?

Nalo lilimgusa Mungu hivi kwamba, hata Yesu akageuka, na kusema, "Ni nani aliyenigusa?"

184 Ndipo Petro akamkasirikia, akamkemea, akasema, "Mbona, Wewe unasema jambo kama hilo? Ujasiri wenyewe! Mbona, kwa nini useme kitu kama hicho? Mbona, kila mtu anakugusa Wewe."

185 Akasema, "Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka." Naye akaangalia moja kwa moja juu ya kusanyiko, karibu hivi, mpaka akampata maskini mwanamke huyo. Akasema, "Imani yako imekuokoa, ninii yako. . . kutokwa na damu kumekwisha." Naye akaja akaanguka chini.

186 Sasa, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli? Sasa, huhitaji kadi ya maombi, kitu pekee unachohitaji ni kumwamini Mungu. Sasa, ninyi huko nje bila kadi zenu za maombi, angalieni *huku*. Nanyi ombeni, na muamini kwa moyo wenu wote. (Hizo ni leso ambazo nitaziombea.)

187 Wewe omba kwa moyo wako wote, useme, "Bwana, Ndugu Branham hanijui, bali Wewe unanijua. Jalia niguse vazi Lako, halafu uzungumze kupitia kwake, jalia aniite hapa kwenye kusanyiko mahali fulani," ambapo-. . . Sijali mahali ulipo, uone kama si sawa kabisa.

188 Halafu, katika mstari huu wa maombi, kadiri ninavyoona hakuna mtu hapo ninayemjua katika mstari huo wa maombi, isipokuwa ingekuwa ni Ndugu Boze aliyesimama pale, nami nafikiri anamsaidia tu Billy. Ni wangapi kwenye mstari huo wa maombi ambao ni wageni kwangu? Inua mkono wako, kwamba unajua sijui lolote kukuhusu. Angalieni hapo.

189 Ni wangapi huko nje wanaojua ya kwamba sijui lolote kuwahusu? Inua mkono wako. Hakuna mtu machoni pangu,

nje ya Ndugu Pat na hawa wengine walioketi hapa, ambao ni—ambao ninawajua katika kusanyiko hilo. Siwezi kumwona mtu ambaye mimi—mimi—mimi . . . Ndugu na Dada Kidd. Nami ninamjua mtu huyu aliyeketi hapa, yeye na mke wake, siwezi kulitaja jina lake, lakini ndugu huyu hapa, mmishenari. Mtu huyo aliyeketi hapo, mimi . . . Dauch, vema. Hiyo ni kweli, hilo jina la Kijerumani, msinifanye . . . Waairishi hawawezi kulitamka jina hilo. Mnaona?

190 Kwa hiyo ninajua yeye ni . . . Nimekutana naye, nami nilimwombea hivi majuzi wakati alipokuwa tu na wakati mbaya sana, naye Bwana akamponya, akaja moja kwa moja mkutanoni huko kwa Ndugu Roberts, kule ilikuwa huko Tulsa, hiyo ni kweli. Mimi . . . Wewe ni mtu yule yule, sivyo?

191 Mnaona, ukisimama hapa juu inakubidi tu kuangalia, na ni vigumu kwako kuona huko nje, kwa sababu nuru zinaangaza moja kwa moja usoni mwangu. Mnaweza kuniona vizuri, lakini ni vigumu kuwaona. Baada ya kupita kama safu moja ama mbili hapa, siwezi kuona chochote, kama tu nukta huko ndani, mahali mnapoketi.

192 Lakini sasa, hawa hapa watu wamesimama nisiowajua, kuna watu huko nje nisiowajua. Lakini huyu hapa Roho Mtakatifu, Yesu Kristo, Yeye ambaye amefufuka katika wafu.

193 Sasa, Yesu alisema nini? Ni wangapi watakaokubali ya kwamba tunaishi katika kizazi kiovu na cha zinaa? Tunaishi. Yesu alisema ya kwamba kizazi hicho kitapokea ishara moja. Hiyo ni kweli? Hiyo ingekuwa ishara gani? Kufufuka kwa Yona. Kweli kabisa, ndugu. "Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku."

194 Basi ni ishara gani hiyo waliyokuwa wapokee? Ishara ya ufufuo. Hiyo ni kweli? Ni wangapi watakubali hilo? Basi kama Yesu Kristo amefufuka katika wafu, Yeye . . . "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Na kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya." Basi ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ndiyo ishara iliyopewa kizazi hiki. Ninasema hivi katika Jina la Yesu: Ipokeeni! Msiogope, ni Kristo. Ikumbatieni, iweni na imani.

195 Bwana, Mungu wa Mbingu na nchi, majira yanasonga mbele, usiku unaingia giza, Nuru ya dunia inazima. Hivi karibuni, Wewe utakuwa hapa, ni giza hivi karibuni, na hakuna mtu anayeweza kufanya kazi. Kutakuwa na mamlaka tawala katika nchi hii ambayo yatafunga mikutano kama hii, hivi karibuni, hatutaweza kuwa na mkutano wa namna hii, hatimaye yatatokea.

196 Ulisema katika Biblia Yako ya kwamba wangeungana pamoja, Wewe ulisema wangeungana, nao wataungana. Na

kutakuja mtikiso mkuu miongoni mwa watu. Na ni wale tu wanaotambuliwa katika shirikisho hili kuu ndio watakaoweza kufanya mikutano. Litakuwa ni kundi la kielimu, Roho atasukumiwa mbali katika uchache. Lakini Wewe ulisema, “Msiogope enyi kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa Ufalme.”

197 Kwa hiyo ninaomba, Baba, ya kwamba wakati kukiwa na Nuru nasi tunatembea, na tuna taifa hili la ajabu tunamoishi, uhuru wa dini, tungali tunaweza kuomba, na bado tuwe na ibada za uponyaji, na kukutumikia Wewe, jalia watu waingie Nuruni wakati Nuru ikiwa hapa. Ninaomba ya kwamba utanitia mafuta usiku wa leo. Nisaidie, Ee Bwana, naomba, katika Jina la Yesu. Amina.

198 [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Um-hum. Vema, tisa na ishirini na moja.) Tisa na ishirini na moja hazipo, tisa na ishirini na moja. Hawako mstarini. Vema, wanaingia, sawa. Hebu. . . Hatuna budi kuanza, maana muda unaenda.

199 Sasa, ni wangapi walioko hapa ambao hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hii hapo kabla? Hebu tuone mkono wako. Angalia tu pale. Sasa, ni wangapi hapa ndani ambao hawajawahi kuwa hapa hapo awali, mmoja wa mikutano yetu, waliowahi kusoma Yohana Mtakatifu 4, yule mwanamke kisimani alipokutana na Bwana Yesu? Hebu tuone mikono yenu, kama hujawahi kuwa hapa hapo kabla. Vema.

200 Sasa, kama Yeye ni Yesu yule yule, hii hapa picha ile ile, mandhari, kile Kisima kipo hapa cha Uzima wa milele, ninaamini hilo. Huyu hapa mwanamke ambaye sijawahi kumwona, na labda hajawahi kuniona. Sisi. . . Aliinua mkono wake hakunijua, wala mimi simjui. Sasa, kama Yeye ni Kristo yeye yule, Yeye atamjua; kama Yeye ni Kristo yeye yule, Yeye ananijua. Na kama akifanya jambo lile lile hapa alilofanya katika Yohana Mtakatifu 4, ni wangapi wenu ninyi wageni mtampokea, na kuamini kwa moyo wenu wote? Inua mkono wako, kama jambo lile lile.

201 Sasa, huyu hapa mimi na huyu mama, hatujawahi kuonana maishani mwetu. Sisi ni. . . Isipokuwa sisi. . . Huenda niliangalia huko nje kwenye kusanyiko, nikamwona; huenda aliangalia mimbarani, na kuniona. Lakini hatufahamiani, sivyo, mama? Hatufahamiani kabisa. Simjui, sijawahi kumwona. Sasa, kama yeye ni mgonjwa, nisingeweza kumponya, Mungu tayari amefanya hivyo, mnaona. Ninaninii tu. . .

202 Sasa, Yesu amesimama hapa amevaa suti hii, aliyowafanya Ndugu Palmer, huko nje mahali fulani, na Dada Palmer kunipa, sasa, kama Yeye alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii, na angesema, naye mwanamke huyu angetembea, na kusema, “Bwana Yesu, ninahitaji uponyaji.”

203 Mnajua kile Yeye angemwambia? “Nilifanya hivyo nilipokufa kwa ajili yako pale Kalvari.” Mnaona?

204 Lakini basi, angejuaje huyo alikuwa ni Yesu? Kwa sababu alikuwa na alama za misumari mkononi Mwake? La, mtu yeyote angeweza kuwa na alama za misumari mkononi mwake. La, la, kumekuwako wengi walioiga hilo. Lakini Yesu halisi angekuwa na...Roho halisi wa Yesu angekuwa ndani Yake, Naye angefanya mambo yale yale aliyofanya kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Hiyo ni kweli?

205 Basi ishara ya Masihi ilikuwa ni nini? Mungu-Nabii. Hiyo ni kweli. Sasa, mnaelewa? Si mimi sasa, ili mpate kulielewa vizuri sana, mimi ni mwanadamu, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, aliye mdogo kuliko wote miongoni mwenu. Hiyo ni kweli. Lakini ni Roho Wake. Unaona?

206 Sasa, kama ninaweza tu kujiachilia...Kama maikrofoni hizi, hizo maikrofoni ni bubu kabisa, isipokuwa mtu fulani anazizungumzia ama kelele fulani, hapana budi pawe na mtetemo wa mawimbi kuipitia; jambo lile lile hapa. Simjui, yeye hanijui. Kama jambo lolote likitukia, itabidi iwe ni mtetemo mwingine wa mawimbi, sivyo? Haina budi kuwa ni Roho Mtakatifu, Kitu pekee angaliweza kuwa.

207 Sasa dada, ili tu kuzungumza nawe. Sasa, kama Bwana Yesu...Kama ningeweza kwenda hapa na kukuwekea mikono, baada ya kuhubiri jinsi nimefanya, na kusema, “Yesu alisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Huo ndio ukweli. Ungeweza kutoka jukwaani, ukisema, “Bwana asifiwe, ninaamini nitapata afya.” Hiyo ni kweli. Unaona? Ungeweza kufanya hivyo.

208 Lakini sasa, vipi kama Yeye akisimama hapa na kukwambia kile umekuwa? Basi kama Yeye anajua kile umekuwa, na kisha akwambie kile utakachokuwa, bila shaka wewe...Kama hiyo ni kweli, unajua kama hiyo ni kweli ama si kweli, basi unaweza kuamini hilo.

209 Hiyo ni kweli, enyi wasikilizaji? Kama anaweza kukwambia kile umekuwa, ama kile kilichokuleta hapa, ama kitu kama tu yule mwanamke aliyekuwa kisimani. Nyote mnaelewa sasa? Bwana na atujalie.

210 Sasa, ninazungumza tu nawe, kwa sababu nimekuwa nikihubiri, ndipo nione tu kama Yeye angeniambia. Kama ataniambia, utamkubali? Ingeisaidia imani yako? Ingekusaidia kuamini?

Itasaidia wasikilizaji kuamini? Mungu wa Mbinguni na alijalie.

211 Sasa, kama kusanyiko lingali linaweza kuisikia sauti yangu, huyo mama, ana shida fulani ambayo inakuja zaidi kama ugonjwa sugu, kwa sababu ninamwona chini ya hema, ama,

hema la oksijeni, ama *chochote kile*, hana budi kupumua kutoka kwenye hema la oksijeni. Ni mzio, hiyo ni kweli kabisa.

212 Yupo m—mtu aliye pamoja nawe, ni mume wako, yupo hapa sasa, naye yuko moyoni mwako. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida ya mumeo? Unaamini? Vema, mume wako anaugua, macho yake yana shida fulani, na pia ana ugonjwa wa damu, ambao unasababishwa na mkanganyiko wa mambo. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

213 Unaamini hilo? Sasa, mwulizeni mwanamke huyo kama hiyo ilikuwa ni kweli. Sijui nilichosema. Jambo pekee mimi. . . Huyo hakuwa ni mimi, huyo alikuwa ni Yeye. Sijui lolote kumhusu, huyo alikuwa ni Yeye. Vema, ulisema. . . Njia pekee nijuayo, ni kwa kanda hizi.

214 Lakini sasa, mnasema, "Vema, labda ulibahatisha."

215 Ngoja kidogo, tutaona, tutaona.

216 Simama tu kwa dakika moja, ninataka kukuuliza jambo fulani, simama tu hapo kwa dakika moja. Wewe ni mtu mzuri, wewe ni Mkristo. Naam, nasikia kitu kikichacharika, ni hema la oksijeni, kitu fulani kuhusu hema la oksijeni. Naam, nami. . . Na mtu fulani, mume wako, naye alitaka kuja hapa, lakini yeye. . . ulikuwa tu na kadi moja ya maombi. Hukujua ni yupi ataichukua, wewe au yeye, kwa hiyo ukaja huku, na, wewe mwenyewe. Sasa, yeye ataponywa, pia, nyote wawili, na nyinyi ni. . . Hiyo ni kweli. Sasa, hilo limetukia tu dakika chache zilizopita.

217 Na hili hapa jambo lingine, ili upate kujua. Kama wewe. . . Hivi unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Hakuna kivuli cha shaka? Unajua ya kwamba kitu Fulani kimekuzunguka, sivyo? Unajua ya kwamba Kitu fulani kinatia mafuta hapa, kitamu sana na kinyenyekevu. Hiyo ni kweli. Hu—hutoki hapa, unatoka mbali na hapa. Unatoka Canada, Ontario. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Nikikwambia wewe ni nani kwa Roho Mtakatifu, itakusaidia? Bibi Buckner, rudi upate afya. Yesu Kristo anakuponya na kukupa afya. Amina.

Unamwamini Bwana Yesu? Mwamini Mungu.

Yote yamekwisha, ndugu. Amini tu sasa.

Hatufahamiani.

218 Sasa, hilo linapaswa kulitatua kwa kundi lote lenu. Je, hilo linathibitisha ya kwamba ninahubiri kweli? Mungu angeniruhusuje kusema jambo ambalo si kweli, na kusimama na Ujumbe wangu wenyewe? Mambo haya ni kuonyesha tu thibitisho la Kiungu kwamba theolojia yangu ni ya kweli. Kweli kabisa. "Neno la Bwana liliwajia manabii."

219 Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Sikujui, Yesu anakujua. Wewe ni mtu mzuri sana, nawe huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, ni binti

yako. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Iko kwenye uti wake wa mgongo. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, unaamini kwa moyo wako wote?

220 Sasa, kumbukeni huo karibu huniua. Hamtambui kile huo unavyokufanyia. Hebu kidogo. Yeye ni mtu mzuri sana, hebu tuzungumze naye tena. Sasa, chochote kile, sijui mimi. Ninii tu. . .Hebu tuone tena. O—ombeni tu. Mnaona? I—iweni tu mkiuliza.

221 Je, yale niliyokwambia yalikuwa ni kweli? Yalikuwa kweli. Naam, naona ni msichana mwenye kitu fulani mgongoni mwake, ugonjwa wa uti wa mgongo. Hiyo ni kweli. Nawe. . .Kuna mtu mwingine, ninamwona mtu akitokea, mtu aliyetiwa uvuli wa mauti, ni mtu unayemwombea, ana kansa. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Kama nikikwambia, itakusaidia? Vema, Bibi Glasgow, nenda zako nyumbani, upate afya, Yesu Kristo anakuponya. Vema, amini, nenda, mwamini Mungu.

222 U—unaamini kwa moyo wako wote? Mwamini Mungu. Unaamini? Hatufahamiani. Kama sikukwambia lolote, nilipita tu na kukuwekea mikono. . .Unajua ya kwamba kitu fulani hapa. . .mimi. . .

223 Yeyote yule, ni nani anayepiga picha, mimi. . .tafadhali, usifanye hivyo tena. Mnaona, Roho Mtakatifu ni Nuru, ninaiangalia papa hapa, nami ninaona hiyo ikimulika sasa. Nami si—si—si—siwezi kumpata, mnaona, siwezi kumshika Roho, anaondoka kwangu. Vema.

224 Sasa, hiyo ni. . .nilimpoteza wakati uo huo. Sasa, hebu kidogo. Sasa, huyu ndiye mgonjwa? Wewe ndiye mgonjwa? Vema. Kama Mungu atanifunulia kilicho shida yako, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Mishipa iliyovimba. Unaamini Yeye anaweza kuiponya? Una kitu kingine unachohofia sana. Hiyo ni kweli. Kama nitakwambia ni nini kupitia kwa Roho Mtakatifu, utaamini ni Kristo amesimama hapa akifanya hivyo? Utaamini?

225 Sasa, jambo fulani lilitukia kwenye kusanyiko wakati uo huo, kuna mtu tofauti aliyetokea hapa. Mnaona? Mtu fulani aliamini kweli, zaidi sana wakati uo huo. Unalia nini, mama? Ilikuwa ni wewe. Vema, unafikiri ugonjwa huo wa matumbo utaondoka sasa? Ni uvimbe. Hiyo ni kweli. *Ilikuwa*. Sikujui. Unaamini kwa moyo wako wote? Mungu akubariki.

226 Yupo mama aliyeketi papo hapo karibu nawe ambaye anaamini kwa moyo wake wote, pia. Uh-huh. Sikujui, mama. Lakini hivi u—u—unamjua Mungu, nawe utamwamini? Kama ninaweza kukwambia shida yako ni nini, utaniamini? Unaugua ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Ni shimo moyoni mwako, ndio kwanza utoke hospitalini. Unatoka Middletown. Unaamini Mungu anakujua? Ann Reed, amini kwa moyo wako wote sasa, na uende nyumbani na uwe mzima. Mwamini Mungu.

227 Unamwamini Mungu? Aligusa nini? Unaona jinsi imani yake inavyojitokeza, moja kwa moja kutoka kwenye kusanyiko hapa? Imani yako ndiyo inayofanya jambo hilo; sijawahi kuwaona watu hao. Sasa, ninyi iweni na imani hapo nje.

228 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani: Aligusa nini? Hawezi kunigusa mimi, yeye—yeye yuko futi thelathini kutoka kwangu, ama arobaini. Lakini aligusa nini? Alikuwa akiamini kwa moyo wake wote, na kuomba, naye akamgusa Kuhani Mkuu. Mimi siye Kuhani Mkuu, Yeye ndiye. Lakini Yeye—Yeye hana midomo ila yangu na yako, Yeye anayo mikono tu kadiri anavyoweza kuitumia, yangu na yako. Wewe amini tu mahali fulani kama hapo, jambo lile lile.

229 Hebu tuone, huyu alikuwa ndiye mgonjwa? Yeye tayari amekwambia shida yako ilikuwa ni nini? Unaamini kama Yeye hajafanya hivyo? Vema. Naam, mishipa iliyovimba, nawe una uvimbe kwenye titi lako. Hiyo ni kweli. Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa nenda nyumbani ukapate afya. Yesu Kristo anakuponya.

Unaamini kwa moyo wako wote kila mtu? Aminini sasa, msiwe na shaka.

U hali gani? Hatufahamiani, nijuavyo mimi. Hiyo ni kweli? Vema.

230 Maskini mama huyo aliyeketi hapo, akiniangalia, akimwombea mumewe, yeye yuko Canada. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Ana kisukari na ugonjwa wa mapafu. Amini kwa moyo wako wote sasa. Mwamini Mungu.

231 Unamwamini Mungu? Ee Mungu, Yehova Mkuu! Unawezaje kutilia shaka? Ninatoa changamoto kwa imani yenu katika Jina la Kristo kuamini ya kwamba nimewaambia kweli!

Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako?

232 Kusanyiko, linaendelea tu...Kuna kitu fulani kinachoendelea kuso-...Iweni na kicho, watulivu, watulivu kweli. Kuna watu wanaoomba, wanaendelea kuja kutoka *huku*, kuna imani nyingi sana humu jengoni usiku wa leo. Kama mtaendelea tu kuamini!

233 Hebu tuone, huyu ndiye mgonjwa? Sijarukwa na akili, ninaninii tu...Hakuna haja ya kujaribu kulielezea, huwezi. Mnaona, hakuna njia ya kujaribu kulielezea, inakubidi tu kuamini. Huwezi kumfafanua Mungu, unamjua Mungu kwa imani.

234 Loo, ni namna fulani ya vipindi ulivyo navyo, kifafa. Ninataka kukwambia jambo fulani lililotukia. Ulipokuwa msichana mdogo, ulianguka na kusababisha jambo hilo, ulipokuwa msichana mdogo. Limekuwa likikusumbua kwa muda mrefu. Unaamini Mungu atakuponya? Hutoki hapa,

unatoka Kusini, Mississippi, Hattiesburg, Mississippi. Unaamini Mungu...? Kama nikikwambia ulikuwa nani, itakusaidia? Binti Sledge, sasa nenda nyumbani, uwe mzima. Yesu Kristo anakuponya.

235 "Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana." Mwamini tu Mungu.

236 Sasa, hatufahamiani, bwana, Mungu anatujua sote wawili. Sasa, kama Bwana Yesu angali anabaki Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye atakujua, ajue yote kukuhusu; mimi sikujui, Yeye anakujua.

Nyote mtaamini hilo, huko nje sasa? Simjui mtu huyo.

237 Umetoka mbali na hapa, umekuja mkutanoni kutoka mahali pengine, Virginia. Amini. Unataka ukombozi kutoka kwa kitu fulani. Hiyo ni kweli, sivyo? Uvutaji sigara, uvutaji sigara. Aisee, mhudumu anapaswa kuachana na jambo hilo. Unataka ukombozi, unajua ni kosa. Bw. Snodgrass, Kasisi Bw. Snodgrass kutoka Virginia, hilo ndilo jina lako. Njoo hapa. Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Nipe mkono wako.

238 Ninaondolea mbali kitu hicho kiovu kutoka kwako kama mwana wa Mungu. Na kikuache na kisirudi tena. Nenda zako ukiamini sasa, na kamwe usivute nyingine maishani mwako mwote. Amina.

Mwaminini Mungu.

239 Unaamini mgongo wako ulipona ulipokuwa umeketi pale? Mgongo wako ulipona ulipokuwa umeketi pale, unaamini hilo? Basi nenda, ukishangilia tu, ukisema, "Asante, Bwana."

240 Maskini mama huyu ndio kwanza ainue mkono wake papo hapo, wakati huo tu. Una jambo fulani niani mwako, sivyo, mama? Unamwombea mwanao, huko ndiko linakotoka. Kuwa na imani. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakupa shauku ya moyo wako.

241 Vema, unaamini hilo...? Vipi kama sikukwambia jambo moja, ungeamini? Ungeamini uliponywa? Umeponywa. Mungu akubariki, nenda zako tu.

Vipi kama sikukwambia lolote, niliweka tu mikono juu yako? Hilo ndilo jambo muhimu kwako, sivyo? Njoo hapa.

Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe. Amina.

Hivyo ndivyo ilivyo rahisi.

242 Mama aliyeketi papa hapa nyuma, maskini mwanamke mwenye nywele nyeusi na amevaa koti jeupe, akimtazama yule mama aliyeketi karibu naye, aliye na yabisi kavu pale, amini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya. Unaamini kwa moyo wako wote? Basi unaweza kuupokea. Hiyo ni kweli, mama. Wewe uliyeinua mkono wako hapo. Hapo, ndivyo hivyo. Simama kwa

miguu yako. Jambo ndilo hilo, simama, ninii tu, haya basi, nenda zako nyumbani, ukaponywe. Yesu Kristo anakuponya.

Wewe pia, dada. Amini kwa moyo wako wote. Nenda na Bwana Yesu akupe afya.

243 Vema, njoo. Mdogo sana kwa huo. Unaamini ugonjwa huo wa anemia utaondoka, na itakuwa sawa? Mungu anaweza kukupa damu kutoka Kalvari kwa ajili yake. Unaamini hilo? Nenda, unaweza kuupokea, katika Jina la Yesu Kristo. Amini sasa kwa moyo wako wote.

Ugonjwa wa moyo, tumbo, loo, jamani, unaamini Mungu atauponya? Nenda ukaamini kwa moyo wako wote, na upate afya.

244 Ni wangapi huko nje mnaoamini kwa moyo wenu wote sasa? Ni wangapi walio katika hali ya . . . unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unaamini kwa moyo wako wote? Uko tayari kupokea uponyaji wako? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba ni Roho Mtakatifu? Ninataka kuona mikono yenu. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba ni Roho Mtakatifu? Kwa moyo wako wote? Pamoja na yote yaliyo ndani yako?

245 Sasa, nitatoa changamoto kwa imani yenu sasa hivi kufanya jambo fulani. Waonaje *wewe*? Waonaje *wewe*? Nyote mnaamini ni Roho Mtakatifu? Ni wangapi wanaojua ya kwamba hayo ni mahubiri yale yale niliyohubiri usiku wa leo ya Yesu Kristo? Ni wangapi wanaoamini ndani na nje? Inueni mikono yenu.

246 Wote watakaomkubali Yesu kama Mponyaji wao sasa hivi, sijali una shida gani, jinsi ulivyolemaa, sijali chochote kuihusu, kama utamkubali Yesu kama Mponyaji wako, simama kwa miguu yako na uinue mikono yako, na uanze kumsifu kwa kukuponya, nawe unaweza kupata uponyaji wako sasa hivi.

247 Bwana Mungu, Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, Ninamwondolea mbali pepo huyu mchafu, ninaondolea mbali nguvu za ibilisi. Na waende nyumbani wakapate afya, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

60-0609 Msiogope
Miami Valley Chautauqua Campgrounds
Chautauqua, Ohio Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org